


Jesus Film Project®
A Cru Ministry

# Kumjua Yesu

## Kuanzisha Jumuiya yako mpya ya Umisheni ukitumia Sinema ya Yesu (*Jesus* Film)

# Kumjua Yesu

## Kuanzisha Jumuiya yako mpya ya Umisheni

Karibuni kwenye Tukio Kuu la kutumia Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film) kuwafikia watu kwa ajili ya Yesu, kuwafunza katika imani, kisha kuanzisha Jumuiya mpya ya imani, na kuizidisha jumuiya hiyo!

v6.5

Jesus Film Project®
A Cru Ministry

Knowing Jesus

# Mungu anataka kukutumia kwa njia ya ajabu kujenga Ufalme wake katika lugha yako kati ya kundi lako la watu.

Mtume Yohana anaandika katika kitabu cha Ufunuo:

9 Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao; 10 wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo. (Ufunuo 7:9-10, SUV)

Ndani ya umati huo watakuwa waabuduo kutoka katika kila lugha na vikundi vya watu ulimwenguni. Watakuwa wakiabudu na kuimba kwa lugha zao wenyewe, na kwa njia zinazoelezea upekee wa tamaduni zao.

Yesu alisema katika mistari ya mwisho ya Injili ya Mathayo:

19 Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; 20 na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari (Matthayo 28:19-20).

Anatuambia ENENDENI, MKAWAFANYE wanafunzi, KUWABATIZA, na KUWAFUNDISHA. Kama tutatii amri yake, basi mahali pazuri panapowezekana kwa wanafunzi hawa kukua ni katika jumuiya au kikundi kidogo cha waamini.

**Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film) ni chombo bora cha kutangaza injili. Unaweza kuionyesha sinema hii kwa majirani, familia na marafiki, na wengi watataka kumfuata Yesu na kuokolewa. Lakini zaidi ya kuwaambia tu kuhusu Yesu, marafiki zako wapendwa na familia wanapokuja kwenye imani unaweza kuendelea kuwajenga katika imani yao kwa kutumia sehemu 61 kutoka katika Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film) ili kuwasaidia kujifunza kuhusu maisha ya Yesu, mafundisho, mifano ambayo Yesu alifundisha, pamoja na miujiza aliyofanya; na pia maombi yake, majaribu, pamoja na kifo na kufufuka kwake.**

# Hatua ya Kwanza 01

**Je, ungependa kuanzisha wapi Jumuiya mpya ya Umisheni?**

**Je, kuna kijiji au mtaa wa karibu ulio karibu ambao unahitaji kumjua Yesu?**

Kwanza, unahitaji kumtambua "Mtu wa Amani" mahali hapo. Katika Luka 10:6, Yesu anawatuma wafuasi wake 72 kupeleka ujumbe wake, wakamtafuta mtu wa amani katika kila mahali walipokwenda na kukaribishwa.
Huyu ni mtu ambaye ana sifa nzuri na ana mtandao wa marafiki na jamaa ambao wanaweza kuwaalika kuja kutazama Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

Tunapendekeza uunde uhusiano wako na mtu huyu, kwa kutumia mchakato wa hatua tatu ambao ni rahisi kukumbuka na ambao utaongoza kwa fursa ya kuwaambia waziwazi juu ya Yesu

### a. Maombi

Tunamuombea mtu huyu wa amani. Omba ili Mungu akuonyeshe ni nani mtu huyo — mtu ambaye ataweza kukutambulisha kwa familia na marafiki zao. Kisha unapoendelea kumfahamu mtu huyu, uliza jinsi unavyoweza kumwombea. Watu wanafurahi kuwapata wafuasi wa Yesu wa kuombea mahitaji yao.
Katika sehemu ya 25 na 26 ya Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film), Yesu anafundisha kuhusu maombi.

### b. Kujali

Tunapoomba kwa ajili ya rafiki huyu mpya na kuanza kuelewa juu ya mahitaji yake, tunaweza kumwonyesha kwamba tunamjali kwa kumsikiliza na kutimiza mahitaji yake ya kimwili. Katika Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film) Sehemu ya 31, Yesu anasimulia habari ya Msamaria Mwema na kufundisha jinsi tunavyopaswa kuwajali majirani zetu. Yesu anaonyesha aina hii ya kujali katika miujiza mingi utakayoyaona kwenye Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film).

### c. Shirikisha

Tunapowasikiliza watu na kusaidia kukutana na mahitaji yao, tunapewa fursa ya kuwashirikisha habari njema za Yesu. Katika Sehemu ya 33 ya Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film), Yesu anafanya urafiki na kumshirikisha Zakayo habari njema.

# Hatua ya Pili

# 02

## Onyesha Sinema ya *Yesu* (*JESUS* Film)

Pamoja na mtu wako wa amani, alika watu 10 au zaidi waje waione Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film), labda nyumbani kwa mtu huyo wa amani. Unaweza kutambua  kuwa wengi zaidi watataka kuja! Katika siku hizi za teknolojia kuna njia nyingi za kuonyesha Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film).

Hapa kuna njia chache:

1. Ikiwa una seti ya vifaa vya Sinema ya Yesu (*JESUS* Film®), vitumie kuunda skrini kubwa, liwe tukio la nje hadharani! Watu wengi watataka kuja kutazama sinema hiyo!

2. Ikiwa unaweza kupata runinga ya skrini bapa yenye kutumia USB, tumia kidunde cha flash drive kuonyesha Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film) katika nyumba ya mtu wako wa amani.

3. Ikiwa una kifaa cha kompyuta au kishikwambi unganisha na spika kwa Bluetooth, unaweza kuonyesha Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film) kwa kundi dogo la watu hadi 20.
Watu watafurahi kuona na kusikia habari za Yesu katika lugha yao wenyewe!

Wakati wa kufunga sinema, toa mialiko miwili kwa kwa watazamaji wako ili wajitoe zaidi.

Kwanza, wape nafasi ya kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi. (Wengi wao watampokea Yesu mara moja!) Pili, waalike warudi siku inayofuata ili kuzungumza zaidi kuhusu Yesu kwa sababu wengine wengi watapendezwa na watakuwa na maswali zaidi.

Sasa ifuatayo ndiyo sehemu bora zaidi!

# Hatua ya Tatu

# 03

## Jumuiya mpya ya Umisheni au Kikundi Kidogo

Bila kujali kama watu walioiona sinema walimpokea Yesu kama Mwokozi wao au la, waalike warudi tena siku inayofuata au jioni ili kuzungumza zaidi kuhusu habari za Yesu.

Katika mkutano huu, (na katika mikutano yote inayofuata), utatumia sehemu 61 za Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film) ili kujifunza zaidi habari za Yesu na kuzungumza juu ya habari zake pamoja nao.

Katika kipindi cha mwaka unaofuata, kikundi chako kipya kitakua katika Kristo. Na, wakiendelea kufanya hivyo, watakua katika upendo wao kwa wao na kuzidisha upendo huo ndani ya jamii yao na katika jamii zingine!

Kutoka kwa mkutano wao wa kwanza kabisa, wanakikundi hawa wapya watapata uzoefu wa maisha katika  Jumuiya mpya ya Umisheni. Tutatumia mfumo wa "Theluthi-tatu" (3/3) kwa kila mkutano.

# Hatua ya Nne

# 04

## Zidisha

Katika Sehemu ya 17 ya Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film), Yesu anafundisha kuhusu kuzaa matunda. Wakati huu kikundi chako kidogo kitakuwa tayari kuamza tena na Hatua ya Kwanza ya kuanzisha jumuiya ingine mpya!

Watakuwa tayari wamejifunza kuhusu nguvu za Yesu juu ya ibilisi, nguvu zake juu ya asili, uwezo wake wa kuponya wagonjwa, kusamehe dhambi, tabia ya mfuasi wa Yesu na matarajio ya Yesu ya kuzaa matunda.

Huenda tayari umekwishamchagua mfuasi mkuu, Timotheo wako, ambaye ataweza kuongoza kundi hili jipya. Msaidie kufuata hatua 1-4 ili kuanzisha kundi jipya la kuzidisha!

Tunaomba kwamba Mungu akubariki unapomwamini ili akutumie kama sehemu ya upanuzi wa ufalme wake mkuu!

## TATU — TATU

Mchakato wa Mafunzo ya Uanafunzi

### Kutazama Nyuma

•Kujaliana sisi kwa sisi. Uliza “mnaendeleaje?”
•Kuabudu
•Kushangilia Uaminifu
•Uwajibikaji na Marudio
•Motisha na Kutia Moyo
•Pandikiza Maono

### Kutazama Juu

•Somo Jipya
•Masomo ya Biblia yenye Msingi wa Utii
•Kujifunza kwa pamoja hadithi mpya kuhusu Yesu

### Kutazama Mbele

•Kujitayarisha kwa ajili ya umisheni
•Kufanyia Hadithi Mazoezi
•Tutashiriki na nani wiki hii?
•Kuombea Utume

# Njia Mbili za Kupitia Mafunzo ya Kumjua Yesu:

Kuna njia mbili za kutumia mtaala huu kuongoza kikundi chako kipya cha umisheni kupitia sehemu za Sinema ya ***YESU*** (***JESUS*** Film).

1. Mwanzo-hadi-Mwisho (Njia ya 1)
Baada ya kuonyesha Sinema ya *YESU* (*JESUS* Film) kwa ukamilifu wake (Hatua ya Pili hapo juu), njia ya kwanza ya kutumia Mafunzo ya Kumjua Yesu ni kuunda kikundi na kuwapitishia wale waliohudhuria Sinema ya *YESU* (*JESUS* film) ukiwaonyesha marudio kwa kuipitia sinema sehemu kwa sehemu, kuanzia mwanzo-mpaka mwisho. Hii ni njia bora ya kutilia mkazo habari na mafundisho yaliopo katika Sinema ya *YESU* (*JESUS* film)!

2. Kujenga Msingi (Njia ya 2)
Njia ya pili ya kutumia Mafunzo ya Kumjua Yesu inahusisha kuwajenga wanachama wapya kwa undani juu ya Imani yao kwa kuanza na baadhi ya kanuni zamsingi. Kwa miaka mingi, Campus Crusade for Christ® (shirika ambalo linatayarisha Sinema ya *YESU* (*JESUS* film), limetayarisha masomo kadhaa yenye kichwa cha “Dhana Zinazohamishika,” ili kusaidia kuwajenga waamini wapya katika imani yao. “Dhana hizi Zinazohamishika,” zimeonyeshwa katika sehemu mbalimbali za Sinema ya *YESU*.

Tafadhali kumbuka kuwa maandishi kamili ya toleo la Dhana Zinazohamishika inaweza pia kusomwa mtandaoni kwenye tovuti ya https://www.cru.org/us/en/train-and-grow/transferable-concepts. unaweza pia kufuatilia kodi hii ya QR kwenye tovuti hiyo:

Kama unatumia Njia ya 2, utafanya kwanza masomo nane yale ya sehemu hii nje ya mpangilio. (Kwenye ukurasa unaofuata kuna orodha ya sehemu 8 na mpangilio uliorekebishwa ambao unapaswa kutumia kuongoza kikundi chako.) Mara tu unapomaliza sehemu hizi nane nje ya mpangilio, rudi kwenye mwanzo wa mtaala wa Kumjua Yesu, na kisha upitie tena kuanzia mwanzo hadi mwisho kwa kufuata utaratibu (kana kwamba unaanza tena kutumia Njia ya 1).

Kwa jinsi hiyo, kiuhalisia utarudia kila moja ya masomo haya manane (kama marudio) kwa mara ya pili.

# Kujenga Msingi (Njia ya 2) kwa Mpangilio wa Sehemu:

Sehemu ya 61 – "Jinsi Unavyoweza Kuwa na Uhakika Wewe Ni Mkristo"
Ikiwa ungekufa leo, je, una uhakika kabisa, bila shaka yoyote, kwamba ungeenda mbinguni? (Hutumia klipu ya "Mwaliko wa Kumjua Yesu Kibinafsi")

Sehemu ya 14 – "Jinsi Unavyoweza Kupata Ujuzi wa Upendo na Msamaha wake Mungu"
Je, wakati fulani unaona vigumu kuamini kwamba unao msamaha kamili wa dhambi zako katika Yesu Kristo? Kiakili unaamini, lakini vipi kuhusu ndani kabisa ya moyo wako? (Tumia klipu ya "Mwanamke Mwenye Dhambi Aliyesamehewa")

Sehemu ya 26 – "Jinsi Unavyoweza Kujazwa Roho Mtakatifu"
Wakristo wengi hawajawahi kusikia ujumbe wenye nguvu na wa kuweka huru juu ya jinsi ya kujazwa na Roho Mtakatifu. (Tumia klipu ya "Kufundisha Kuhusu Maombi na Imani")

Sehemu ya 8 – "Jinsi Unavyoweza Kuwa Shahidi Mwenye Kuzaa Matunda"
Wakristo wengi wanashangaa kwa nini hawaoni watu wengine wakija kumjua Kristo. Hata hivyo, tunaweza kuwa na mvuto wenye kuzaa matunda kwa Yesu popote tuendapo. (Tumia klipu ya "Kuvua Samaki kwa Kimuujiza")

Sehemu ya 60 – "Jinsi Unavyoweza Kusaidia Kutimiza Agizo Kuu"
Habari njema inapaswa kupelekwa kwa kila taifa: nguvu ya injili na furaha ya kuwaambia watu kuhusu Yesu. (Tumia klipu ya "Agizo Kuu na Kupaa Mbinguni")

Sehemu ya 31 – "Jinsi Unavyoweza Kupenda Kwa Imani"
Mfano wa Msamaria Mwema unaonyesha nafasi kubwa ya imani katika kuwapenda wengine. (Hutumia klipu ya "Mfano wa Msamaria Mwema")

Sehemu ya 25 – "Jinsi Unavyoweza Kuomba kwa Ujasiri"
Je, umewahi kufikiria kwamba unaweza kumpata mara moja Mtu mwenye nguvu zaidi katika ulimwengu wote mzima? (Tumia klipu ya "Sala ya Bwana")

Sehemu ya 38 – "Jinsi Unavyoweza Kupata Furaha ya Utoaji"
Mojawapo ya matukio ya kusisimua unayoweza kupata ni ujuzi wa kutoa kwa imani. (Tumia klipu ya "Sadaka ya Mjane")

# Sehemu ya 1: Mwanzo – Kitabu cha Mwanzo

Kutazama Nyuma

## Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

## Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

## Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

## Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

## Utangulizi

Sehemu hii ya Sinema ya *YESU* (*JESUS* film) inatueleza jinsi Mungu alivyoumba ulimwengu wote ikiwa ni pamoja na Dunia, mimea, wanyama na binadamu. Inasimulia habari ya jinsi Adamu na Hawa walivyotenda dhambi na kumwasi Mungu na matokeo ya dhambi yao. Tunajifunza jinsi Mungu alivyotoa ahadi kwa Abrahamu na kuahidi Mwokozi ambaye angeondoa dhambi ya ulimwengu.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Biblia huanza na uumbaji wa vitu vyote. Kwa nini Dunia ni muhimu katika mpango wa Mungu?
3. Maandiko yanasema nini sababu ya Mungu kuwaumba Adamu na Hawa?
4. Ni nini kiliwapata Adamu na Hawa? Je, matokeo ya matendo yao katika bustani yalikuwa yapi?
5. Kwa sababu Mungu bado aliwapenda wanadamu, alikuwa na mpango wa kuwarudisha katika uhusiano na Yeye mwenyewe. Ni tukio gani katika maisha ya Abrahamu (katika sehemu hii ya sinema) inaonyesha ni nini kingehusika katika mpango huo wa Mungu?
6. Mungu aliahidi ni nani angekuja kama dhabihu ya dhambi kwa ajili ya watu wake?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

## Tamati

Mungu aliwaumba wanadamu kwa mfano wake ili wampende na kumfurahia Yeye, lakini watu walitenda dhambi dhidi ya Mungu na kutengwa naye. Mungu alikuwa na mpango wa kuwarudisha watu katika uhusiano naye. Mpango huu ulimhusisha Masihi aliyeahidiwa: Yesu Kristo, ambaye angelipa adhabu ya dhambi.

---

Kutazama Mbele

## Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 2: Kuzaliwa kwa Yesu (Luka 1:26-33, 2:1-7)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Kila mtu ana siku ya kuzaliwa. Kila mtu huingia maishani kwa njia ile ile. Hata Yesu. Yesu ni Mwana wa Mungu ambaye alichagua kujifananisha na wanadamu kwa kuja ulimwenguni kwa njia sawa na kila mtu mwingine. Alifanya hivi ili kushiriki nasi ubinadamu wetu na kuonyesha kwamba Yeye si Mungu tu bali kwamba ni Mwanadamu wa kweli pia.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia habari ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, Mariamu aliitikiaje maneno ya malaika kwamba angemzaa Masihi?
3. Unafikiri ni kwa nini malaika Gabrieli alisema mtoto huyo angekuwa Mtoto Mtakatifu?
4. Kwa nini unafikiri ni muhimu kwamba Yesu alizaliwa na bikira?
5. Kwa nini ilikuwa muhimu kwa Yesu kuzaliwa Bethlehemu? (Soma Mika 5:2)
6. Maria na Yusufu walimtumainije Mungu katika matukio yaliyohusu kuzaliwa kwa Yesu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

- Ilikuwa ni mimba ya Yesu ambayo ilikuwa ya kipekee, si tu kuzaliwa kwake tu.
- Mariamu na Yusufu wote wawili walimtumaini Mungu wakati wa kuzaliwa kwa Yesu.
- Yesu alikuwa Mungu na Mwanadamu kama inavyothibitishwa na kuzaliwa kwake na bikira Mariamu.
- Yesu, Mwana, aliishi pamoja na Baba kabla ya kuumbwa ulimwengu, malaika, au kiumbe kingine kilichoumbwa.

### Swali la Matumizi

Je, Sehemu hii imebadilisha mawazo yako kuhusu unavyofikiri Yesu ni nani? Ikiwa ndivyo, kwa njia zipi?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 3: Utoto wa Yesu (Luka 2:41-52)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Yesu alituachia mfano wa jinsi ya kukua katika maisha yetu ya kibinafsi. Kifungu hiki kinaonyesha kwamba alikuwa mtiifu kwa wazazi wake; Alikuwa mtiifu kwa Mungu na akakua katika tabia na katika heshima kwa Mungu na wanadamu. Somo mojawapo ambalo tunaweza kujifunza ni kwamba ni muhimu kuendelea kuboresha tabia zetu katika safari hii ya maisha.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia habari ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je Mzee (Simeoni) anasema nini kuhusu Yesu?
3. Yesu aliwashangazaje walimu? Kwa nini hii haingekuwa jambo la kawaida?
4. Je, kifungu hiki kinaonyeshaje kwamba Yesu si Mungu tu bali pia, “Mwanadamu mkamilifu?”
5. Je, Mariamu na Yusufu walionyeshaje kwamba walikuwa wakimlea Yesu kwa usahihi kulingana na desturi za kidini zilizoelezwa katika Agano la Kale?
6. Yesu anamwita Mungujina gani? Je, hii inatuambia nini kuhusu kile alichojua Mwenyewe katika umri huu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Yusufu na Mariamu walimtii Mungu kwa jinsi walivyomlea Yesu kwa kumpeleka kwenye sikukuu ya Pasaka, na basi wakatuachia mfano mzuri wa malezi. Tunajua kutoka katika Biblia kwamba Yesu alijua misheni yake maishani alipokuwa na umri wa miaka 12. Mungu alituachia simulizi hili la utoto wa Yesu ili kuonyesha jinsi alivyokua, lakini mengi ya yaliyoandikwa kumhusu yahusu maisha yake ya utu uzima na huduma, mambo ambayo Mungu anataka tujue.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 4: Ubatizo wa Yesu na Yohana (Luka 3:21-22)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Sehemu hii ya Luka inaanzisha huduma ya Yesu ya hadharani. Yesu alikuwa ametembea kutoka Galilaya hadi mto Yordani ili abatizwe na Yohana. Yesu hakubatizwa na Yohana ili kuonyesha huzuni yoyote kwa ajili ya dhambi yake, kwa sababu hakutenda dhambi kamwe. Alibatizwa ili kuonyesha kwa ulimwengu wote kwamba alikuwa akituwakilisha katika maisha yake yote, na pia katika kifo chake.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia habari ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri Yohana alikuwa anazungumzia nini aliposema watu wanapaswa "kutubu"?
3. Kwa kuwa Yesu hakuwahi kufanya dhambi, unafikiri kwa nini alitaka kubatizwa?
4. Mungu alipozungumza kutoka mbinguni, unafikiri kwa nini Mungu alipendezwa na Yesu?
5. Biblia inafundisha kwamba Mungu anadumu katika nafsi tatu, lakini Yeye ni mmoja. Hii inaitwa "Utatu." Je, unaweza kupata washiriki wote watatu wa Utatu katika kifungu hiki? Je, ni akina nani?
6. Yohana anasema nini litakuwa kusudi la Yesu maishani?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Yesu hakuhitaji kubatizwa kwa ajili ya dhambi yoyote, alibatizwa ili awe mmoja na watu. Katika Biblia "toba" ina maana ya kubadili mawazo yako kuhusu Yesu na kuishi kwa njia mpya. Tunajifunza hapa kwamba kusudi la huduma ya Yesu ni kuondoa dhambi ya ulimwengu.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 5: Ibilisi Anamjaribu Yesu (Luka 4:1-13)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Ni nini kinachomfanya Yesu awe wa pekee kati ya kila mtu ambaye amewahi kuishi? Je, yalikuwa ni mafundisho yake? Miujiza yake? Pengine, lakini moja ya mambo ambayo yanamtenganisha Yesu na kila mtu mwingine ni ukweli kwamba hakuwahi kutenda dhambi, ama kwa yale aliyosema au aliyofanya. Ingawa ibilisi alijaribu kumfanya Yesu atende dhambi, hakufanikiwa. Hii ni mara ya kwanza ibilisi anatajwa katika Jipya Agano. Kama angaliweza kumfanya Yesu atende dhambi, (kama alivyofanya kwa Adamu na Hawa), ibilisi angeharibu mpango wa Mungu wa kuwaokoa wanadamu.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia habari ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Eleza njia ambazo ibilisi alimjaribu Yesu.
3. Kwa nini ni muhimu kwamba Yesu alinukuu Biblia kwa ibilisi alipojaribiwa?
4. Ukweli kwamba Yesu alipinga kishawishi unathibitishaje kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu?
5. Kwa nini unafikiri ni muhimu kwamba Yesu hakuwa na dhambi?
6. Tunapaswa kufanya nini tunapojaribiwa?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Yesu anathibitisha kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu kwa kutokuwa na dhambi maishani mwake. Yesu ananukuu kutoka katika Biblia ili kumsaidia kushinda majaribu. Ibilisi alimjaribu Yesu alipokuwa dhaifu. Ibilisi anaendelea kuwajaribu watu katika maeneo mbalimbali ya maisha. Kwa hiyo, Yesu anaweza kutusaidia tunapojaribiwa.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 6: Yesu Anatangaza kutimizwa kwa Maandiko (Luka 4:16-30)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Watu wana kujitolea kwa aina tofauti kwa Yesu. Baadhi ya watu hukubali mafundisho yake lakini hawakubali wokovu anaoutoa. Wengine hawafikiri kamwe juu ya Yesu kabisa. Na cha kusikitisha ni kwamba, baadhi ya watu wanamkataa, kama walivyofanya watu katika mji wake mwenyewe wa Nazareti.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia habari ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Yesu alikuwa akisema nini kuhusu yeye mwenyewe aliposoma kutoka katika kifungu cha Isaya 61?
3. Je unafikiri kifungu hicho kinatuambia nini kuhusu Yesu kwamba anawajali maskini, vipofu, wafungwa na wanaokandamizwa?
4. Yesu anapotumia maneno "habari njema" katika mstari wa 18, unafikiri anamaanisha nini? Je, unajua neno lingine ambalo Biblia hutumia linalomaanisha, "habari njema"?
5. Yesu anataja katika mstari wa 18 kwamba "Roho wa Bwana yu juu yangu." Je ni wapi pengine hadi sasa ambapo tumeona Roho Mtakatifu katika maisha ya Yesu?
6. Je unafikiri ni kwa nini watu walimkataa Yesu? Kumkataa kwao kunaonyesha nini kuhusu mioyo yao? Je, walichukua hatua gani dhidi ya Yesu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Yesu alianza huduma Yake ya hadharani kwa kudhihirisha kuwa alikuwa Masihi wa Agano la Kale. Yesu anajali mahitaji ya watu ya kimwili na ya kiroho pia. Mungu anataka watu wamwamini Mwana wake ili waweze kuokolewa kutoka katika dhambi zao na kuingia katika Ufalme wake.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 7: Mfano wa Mfarisayo na Mtoza Ushuru (Luka 18:9-14)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Je, watu kwa kawaida humkaribia Mungu  vipi? Kuna njia mbili kimsingi: aidha kwa kutii orodha ya sheria au kwa kuwa na imani. Kila dini isipokuwa Ukristo ina orodha au kanuni ambazo mtu anapaswa kuzifuata ili kupatana na Mungu. Ukristo, kinyume chake, ndio mfumo pekee wa kiimani unaomkaribia Mungu kwa njia ya imani… si kwa kushika sheria ili kupata kibali chake. Ukristo unakubali kile ambacho Mungu ametufanyia katika Kristo kama njia pekee ya kukubalika na Mungu. Katika sehemu hii tunayokaribia kutazama, "Farisayo" ni kiongozi wa kidini katika Israeli ambaye alikuwa na jukumu la kuwafundisha watu kuhusu Mungu. Walipaswa kushika kanuni na sheria nyingi. Hilo liliwafanya wajione kuwa bora kuliko watu ambao walipaswa kuwatunza.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Watoza ushuru walichukiwa na watu wa Israeli kwa sababu walifanya kazi kwa ajili kwa ajili ya serikali tawala ya Warumi na kuwafanya watu walipe viwango vya juu vya kodi. Kwa nini wewe unafikiri Yesu alichagua mtoza ushuru kwa hadithi hii?
3. Farisayo ana mtazamo gani anapoomba? Kwanini anadharau watu wengine?
4. Mtazamo wa mtoza ushuru ni upi? Anamwomba Mungu amfanyie nini?
5. Je, unafikiri neno "kuhesabiwa haki" linamaanisha nini? (Ona Warumi 5:1)
6. Ni yupi kati ya wanaume wawili katika habari unafikiri alienda nyumbani akiwa sawa na Mungu? Kwa nini?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Ukristo hauhitaji mwanadamu kushika kanuni zozote ili kuwa sawa na Mungu. Inahitaji imani tu. Kiburi huwaweka watu mbali na Mungu kwa sababu wanajiamini badala ya kumtegemea Mungu. Mungu huwapa rehema watu wanyenyekevu wanapomwomba.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 8: Kuvua Samaki Kimuujiza (Luka 5:1-11)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi – Jinsi Unaweza Kuwa Shahidi Mwaminifu

Yesu alifanya muujiza huu ili kuwaonyesha wanafunzi Wake kwamba Yeye ndiye Masihi, na kwamba walipaswa kumfuata na kuwa "wavuvi wa watu." Walitambua kwamba Yesu ndiye Masihi, na wakaziacha nyavu zao na kumfuata. Hakuna jambo maishani linalosisimua na lililo na faida zaidi kiroho kuliko tukio la kuvua watu. Unapofuata maagizo ya Yesu, nyavu zako pia zaweza kujazwa—hata kama hujawahi kumleta mtu yeyote kwa Kristo. Unaweza kuwa na shaka kama Petro. Lakini kama wewe ni mtiifu, Bwana atakutumia kuwaongoza watu wengi kuwa wafuasi wa Yesu.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake mwenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Yesu alimwomba Petro afanye nini? Ilikuwa ni pendekezo au amri? Jambo hili linasema nini kuhusu Yesu?
3. Petro aliitikiaje maneno ya Yesu?
4. Unafikiri kwa nini Petro alisema kwamba alikuwa "mtu mwenye dhambi"? Kwa nini alimwomba Yesu aondoke kwake baada ya kuvua samaki kimuujiza?
5. Petro, Yakobo, na Yohana walionyeshaje kujitolea kwao kwa Yesu?
6. Unafikiri Yesu alimaanisha nini aliposema wangekuwa "wavuvi wa watu"?
7. Baadhi ya mambo ambayo yanaweza kukuzuia kuzungumza na wengine kuhusu Yesu ni yapi?
8. Yesu anawaambia "Msiogope." Unafikiri wanafunzi wanaweza kuwa waliogopa nini baada ya kushuhudia muujiza na kusikia maneno ya Yesu kwao?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Ili uwe shahidi mwenye matunda, unahitaji kuwa na uhakika kwamba wewe ni Mkristo na kwamba hakuna dhambi ambayo haijatubiwa maishani mwako. Ni lazima ujazwe na Roho Mtakatifu. Haya ni mafundisho kutoka kwenye masomo yetu ya awali. Mwisho, lazima uwe tayari kushirikisha imani yako kwa kujifunza habari ya injili. Unaweza kusimulia habari kwa maneno yako mwenyewe au kuonyesha sehemu ya mwisho kutoka kwa Sinema ya Yesu (Jesus Film) kwa rafiki au jirani anayehitaji kumjua Yesu. La muhimu zaidi, unahitaji kuwapenda watu na kuchukua hatua ya KWENDA na KUSEMA habari njema. Ombea fursa na umtarajie Mungu akutumie.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.
Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 9: Binti wa Yairo Arejeshewa Uhai Wake (Luka 8:40-42, 49-56)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Huzuni ni hisia ya kawaida ya mwanadamu. Katika habari hii baba anaomboleza kwa sababu binti yake, ambaye alikuwa mgonjwa, sasa amekufa. Alikuwa amemwomba Yesu aje kumponya, lakini sasa amechelewa. Yesu, hata hivyo, anamwambia mtu huyo aamini tu na asiogope. Kisha Yesu alimfufua binti kutoka kwa wafu, akamaliza maombolezo ya baba yake. Jambo la ajabu kuhusu Yesu ni kwamba ingawa hatatufanyia muujiza wa ufufuo wakati tunahuzunika, anaweza kuponya mioyo yetu na kutusaidia wakatiwa majonzi na huzuni.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri ni kwa nini Yairo alimsihi Yesu aje kumsaidia binti yake? Je, hii inaweza kusema nini kuhusu jinsi alivyomwona Yesu?
3. Yesu alimwambia nini Yairo alipojua kwamba binti yake alikuwa amekufa?
4. Wazazi wa msichana huyo waliitikiaje Yesu aliposema msichana hakuwa amekufa bali amelala? Unafikiri ni kwa nini Yesu alisema hivi?
5. Jambo hili linaonyesha nini kuhusu Yesu kwamba anaweza kuwafufua wafu?
6. Unafikiri Petro, Yakobo na Yohana walifikiri nini walipoona muujiza huu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Yesu anaweza kufufua watu kutoka kwa wafu, akithibitisha tena kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu. Yesu ana huruma kwa wale wanaohuzunika. Yesu ana uwezo wa kutusaidia katika hofu zetu za kifo na kupoteza. Yesu anatuomba tuamini kwamba anaweza kutusaidia katika majaribu na magumu yetu.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 10: Wanafunzi Wachaguliwa (Luka 6:12-16)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Ilikuwa ni nia ya Yesu kila mara kufanya huduma yake iendelezwe na wafuasi mahususi aliowachagua na kuwaita “mitume.” Neno hili linamaanisha “waliotumwa” Tofauti na jinsi tungeweza kuwachagua, Yesu alichagua wanaume ambao walikuwa na elimu ya chini, waliofanya kazi ngumu, waliotambuliwa kuwa “wenye dhambi,” na wakati mwingine walikuwa dhaifu katika imani na kujitoa kwao kwake. Hii inatuonyesha kwamba Yesu anaweza kumtumia yeyote ikiwa yuko tayari kumfuata.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri ni kwa nini Yesu alitumia usiku kucha kumwomba Mungu kabla hajawachagua mitume wake kumi na wawili?
3. Yesu alimchagua Mathayo, mtoza ushuru aliyechukiwa na watu wa nchi yake. Je, hii inasema nini kuhusu Yesu?
4. Unadhani kwa nini Mathayo aliinuka kutoka kwenye lango la ushuru na kumfuata Yesu? Huenda Mathayo aliacha nini ili kumfuata Yesu?
5. Kwa nini Mathayo, baada ya kuitwa na Yesu, aliandaa chakula cha jioni na kuwaalika marafiki zake wote waje kukutana na Yesu?
6. Neno “mtume” maana yake ni “waliotumwa.” Kutokana na yale ambayo umejifunza hadi sasa, ujumbe wa mitume ungekuwaje walipoenda nje kuhudumu?

### Tamati

Ikiwa maombi yalikuwa muhimu kwa Yesu, kadhalika ni lazima iwe muhimu kwetu pia. Yesu alichagua watu wa kawaida, hata wenye dhambi, kuwa Mitume Wake. Yesu huwatumia watu kuendeleza huduma yake. Yesu anataka tuwatambulishe watu Kwake, kama Mathayo alivyofanya.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 11: Heri (Luka 6:20-27)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Yesu anataka wale wanaomwamini wamfuate pia. Anajua kwamba tunajisikia kutoshelezwa na kubarikiwa zaidi tunapomfuata na kutii amri zake. Katika sehemu hii ya kitabu cha Luka, Yesu anaeleza jinsi watu wanavyopaswa kujifikiria kabla ya kuwa wafuasi wake. Anawaelezea wafuasi wake kama “maskini” na wale “wenye njaa.” Tutaona kwamba maneno haya mawili yanaelezea mtazamo wa moyo unaomkubali Yesu kama Mwokozi na kufungua mlango wa kumfuata kama Bwana.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Yesu anapozungumza kuhusu “maskini wa roho,” anazungumzia watu ambao ni maskini kiroho badala ya maskini wa kifedha. Unafikiri inamaanisha nini kuwa “maskini wa kiroho”?
3. Vivyo hivyo, Yesu anapozungumza kuhusu wale “walio na njaa,” anazungumzia njaa ya kiroho badala ya njaa ya kimwili. Unafikiri inamaanisha nini kuwa na njaa ya kiroho?
4. Kutakuwa na nyakati ambazo Wakristo hawatapendwa na wale ambao si Wakristo. Wakristo wanapaswa kufanya nini wanapotendewa vibaya?
5. Yesu anasema wafuasi wake “wamebarikiwa” wakiteswa. Je, mtu anayeteswa anawezaje kuwa aliyebarikiwa?
6. Kwa nini inaweza kuwa vigumu kwa wale walio matajiri katika mambo ya ulimwengu huu kumtumaini Yesu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Kuwa mfuasi wa Yesu maana yake ni kuwa mnyenyekevu moyoni mwako. Kuwa mfuasi wa Yesu kunamaanisha kwamba utapata maana na amani katika kutii amri zake. Kuwa mfuasi wa Yesu maana yake ni kwamba utasamehe wale wanaokutendea mabaya. Kuwa mfuasi wa Yesu maana yake ni kutazamia mbinguni ambako utapata thawabu yako.

---

**Kutazama Mbele**

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.

# Sehemu ya 12: Hotuba ya Mlimani (Luka 6:24-46)

Kutazama Nyuma

## Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

## Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

## Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

## Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

## Utangulizi

Watu wengi wanamsifu Yesu. Watu wengi husifu mafundisho Yake. Watu wengi huenda kanisani kwa sababu wanafikiri hivyo ndivyo Yesu anataka kutoka kwao. Lakini Yesu anasema kwamba wale wanaompenda na kumfuata watafanya kile anachosema. Hasemi hivi ili watu waweze kufika mbinguni kwa kuyatii mafundisho yake, bali ili awatosheleze na kuyabariki maisha yao wanapofanya bidii kumtii Yeye. Mafundisho yake katika Hotuba ya Mlimani yanaeleza sifa za wale wanaotafuta kumfuata Yesu na kuyatii mafundisho yake.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.

Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.

Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.

Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Kwa nini unafikiri watu wanataka kuwa matajiri? Unafikiri ni kwa nini Yesu alitumia muda mwingi kuzungumza kuhusu fedha?
3. Je, watu waliomsikia Yesu akihubiri waliitikiaje kwake?
4. Neno “rehema” linamaanisha nini? Unafikiri Mungu huwaonyesha watu rehema kwa jinsi gani?
5. Kwa nini ni vigumu kuwasamehe watu wanapofanya mambo ya kukuumiza? Je, ni vigumu kwa Mungu kutusamehe?
6. Kulingana na mafundisho ya Yesu katika kifungu hiki, kwa nini unafikiri ni makosa kuwashutumu na kuwahukumu watu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

## Tamati

Yesu anaonya tena jinsi utajiri unavyoweza kukuweka nje ya mbingu. Yesu anatukumbusha kwamba Mungu ni mwenye rehema na sisi pia tunapaswa kuwaonyesha wengine rehema. Yesu anatukumbusha kuwasamehe wengine kwa sababu nasi tumesamehewa. Yesu anaonya dhidi ya kuwahukumu wengine na kuwa wanafiki kwa sababu tunaweza kuwa sawa na wale tunaowahukumu.

---

Kutazama Mbele

## Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

**Sehemu hii ya 13: Haijajumlishwa.**

**Sehemu hii ni fupi na haina kifungu cha Biblia cha kujifunza.**

**Endelea na sehemu ya 14.**

## Sehemu ya 14: Mwanamke Mwenye Dhambi Asamehewa (Luka 7:36-50)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

Kutazama Juu

### Utangulizi – Jinsi Unavyoweza Kupata Ujuzi wa Upendo na Msamaha wa Mungu

Yesu aliwapenda na kukaa pamoja na watoza ushuru, makahaba na wagonjwa. (Siku zile wagonjwa walionekana kuwa wenye dhambi kwa sababu ya ugonjwa wao.) Yesu hakuwahi kuwahukumu watu hawa; kwa hakika, watu pekee aliowahukumu walikuwa viongozi wa kidini waliojiona bora kuliko wengine. Viongozi hao wa kidini waliweka mkazo sheria na kanuni hususa zinazoitwa "Sheria" ambazo watu walipaswa kushika ili kupata msamaha na kibali cha Mungu. Biblia inatuambia kwamba Yesu Kristo, kupitia kifo chake msalabani, ametuweka huru — huru kutokana na dhambi, tukawa huru kutokana na kupata kibali cha Mungu kwa matendo yetu wenyewe, na tukawa huru kutokana na utumwa wa hatia unaotokana na kutoweza kwetu kutii yote ambayo "Sheria" ilidai.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Kwa nini unafikiri mwanamke alikuwa akilia?
3. Farisayo aliitikiaje kwa kile mwanamke huyo alichofanya? Ilikuwaje tofauti kutokana na jinsi Yesu alivyotenda?
4. Hadithi ya msamaha ambayo Yesu alimwambia Farisayo ilikuwa na maana gani?
5. Mwanamke alionyeshaje kwamba alimwamini Yesu?
6. Unafikiri ni kwa nini Simoni hakumpa Yesu ukarimu wowote?
7. Yesu anapomwambia yule mwanamke "imani yako imekuokoa," unafikiri aliokolewa kutokana na nini?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Ili kupata msamaha kama huyu mwanamke katika hadithi hii, lazima "upumue kiroho." Unapumua nje kiroho unapoungama dhambi zako kwa imani. Biblia inaahidi kwamba ukiziungama dhambi zako kwake, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata kukusamehe na kukusafisha na udhalimu wote (1 Yohana 1:9). Kwanza, unakubali kwamba dhambi zako ni mbaya na zinamhuzunisha Mungu. Pili, unatambua kwamba Mungu tayari amekusamehe dhambi zako kupitia kifo cha Kristo na kumwaga damu yake msalabani. Tatu, unatubu. Unabadilisha mtazamo wako, ambayo husababisha mabadiliko ya vitendo. Kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, unageuka kutoka kwenye dhambi zako na kubadilisha mwenendo wako. Katika somo la sehemu ya 26, tutajifunza kuhusu sehemu ya pili ya kupumua ndani kiroho: Kuvuta pumzi, kujazwa Roho Mtakatifu.

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.

# Sehemu ya 15: Wanafunzi Wanawake (Luka 8:1-3)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Katika siku za Yesu hadhi ya wanawake ilikuwa ya chini sana. Katika utamaduni wa Wayunani, mara nyingi wanawake walionekana kama vifaa vya kutumiwa kujifurahisha. Wengi waliamini Sheria ilisema wanawake ni duni kuliko wanaume. Kwa hakika, Agano la Kale linatoa hadhi na usalama kwa wanawake wa Israeli. Hata hivyo, katika utamaduni wa Kiyahudi, wanawake walikuwa chini ya mamlaka ya wanaume na walionekana kuwa sawa na watumwa na watoto wadogo. Yesu aliwathamini wanawake, jambo ambalo lilimweka kuwa kinyume na utamaduni wake.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, ungejisikiaje ikiwa ungekuwa mmoja wa wale walioponywa na Yesu?
3. Je hili linatuambia nini kuhusu wale wanawake waliomfuata Yesu kwamba waliitegemeza huduma ya Yesu kwa kutoa fedha zao?
4. Je, Wanafunzi 12 walikuwa wakijifunza nini kwa kuwa pamoja na Yesu ambacho kingewasaidia baadaye katika huduma yao kwa ajili yake?
5. Je hili linatuambia nini kuhusu Yesu kwamba aliwaruhusu wanawake wamtumikie na kuwaruhusu wamfuate alipofundisha na alipoponya watu?
6. Fikiria jinsi wanawake kwa ujumla wanavyotazamwa katika jamii yako. Je, utamaduni wako ukoje ukiulinganisha na jinsi Yesu alivyowatendea au kuwaona wanawake?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Mtazamo wa Yesu juu ya wanawake ulikuwa tofauti kabisa na ule wa utamaduni wa Wayunani, wa Kirumi au wa Kiyahudi. Yesu aliwaruhusu wanawake kusafiri pamoja naye, kumtegemeza na kumhudumia. Yesu alituwekea mfano wa kuwatendea wanawake kwa heshima, utu na upendo.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) ya mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 16: Yohana Mbatizaji Gerezani (Luka 7:18-23)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Jamii yetu ingemkaribia Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Ni kawaida kwa Wakristo kuwa na mashaka. Kwa sababu tunaishi katika ulimwengu wenye dhambi, na bado hata sisi tunasumbuliwa na dhambi zetu, hakika tutakuwa na mashaka. Tunaweza kuwa na shaka kama Mungu anatupenda, tunaweza kuwa na shaka kama Mungu atatutunza, na tunaweza kuwa na shaka ikiwa Biblia ni ya kweli. Sehemu hii inaonyesha kwamba hata Yohana Mbatizaji alikuwa na mashaka kuhusu Yesu alikuwa nani. Yesu anaweza kutusaidiakatika mashaka yetu, kama alivyomsaidia Yohana Mbatizaji.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Kwa nini Yohana aliwatuma wanafunzi wake wawili kwa Yesu? Unafikiri Yohana alikuwa anatarajia kusikia nini?
3. Kwa nini unafikiri ilikuwa muhimu kwa Yesu kufanya miujiza mapema katika huduma yake?
4. Kwa nini Yesu anawajibu wanaume waliotoka kwa Yohana kwa kuyataja yale aliyoyafanya (kuponya wagonjwa, vipofu, viwete)? Kwa nini asijibu tu, Ndiyo, Mimi Ndiye yule?
5. Ingawa huenda Yohana alikuwa na mashaka yake mwenyewe, Yesu anamwelezaje?
6. Ilimbidi Yohana kutegemea kusikia kuhusu huduma ya Yesu tofauti na kumwona Yesu akihudumu. Kujifunza kuhusu miujiza ya Yesu katika Biblia kunaweza kutusaidiaje kumwamini?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Shaka na imani huambatana. Hakuna mtu aliye na imani kamilifu. Miujiza ya Yesu ni ushahidi kwamba Yeye ndiye Masihi, Yule ambaye Yohana Mbatizaji alikuwa akimngoja. Yesu alifanya miujiza mapema katika huduma yake ili kuthibitisha kuwa alikuwa Masihi. Alifanya miujiza michache na kufundisha zaidi wakati huduma yake ilivyoendelea. Inawezekana kuamini miujiza ya Yesu, hata kama hujaiona, kwa sababu Biblia ni habari ya kweli ya maisha ya Yesu.

### Swali la Matumizi

Je, Sehemu hii imebadilisha mawazo yako kuhusu unavyofikiri Yesu ni nani? Ikiwa ndivyo, kwa njia zipi?

---

**Kutazama Mbele**

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chemu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.

# Sehemu ya 17: Mfano wa Mpanzi na Mbegu (Luka 8:4-15)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Yesu alifundisha watu kupitia mahubiri, kupitia maswali na majibu na kwa “mifano.” Mifano ilikuwa mlinganisho uliopanuliwa au ulinganisho uliovuviwa na ilikuwa njia ya kawaida Yesu alipofundisha wengine kupitia kusimulia hadithi. Njia nyingine ya kueleza mfano ni kwamba ni “habari ya duniani yenye maana ya mbinguni.”

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, ni aina gani nne ya udongo ambao Yesu anazungumzia katika mfano huu? Yesu anasema kila moja ya udongo huo unawakilisha nini?
3. Unafikiri Yesu anamaanisha nini anaposema, “Mwenye masikio ya kusikia, na asikie?”
4. Ni majaribu ya aina gani yanawza kufanya watu kuachana na imani yao kwa Mungu
5. Yesu anasema udongo mwema utazaa matunda mengi. Hapa Yesu anasema kuhusu tunda gani la kiroho?
6. Tunaweza kufanya nini ili kuandaa udongo wetu ili kwamba Mungu aweze kutoa matunda kutoka maishani mwetu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Yesu anaeleza kwa nini watu wengine wanaamini na wengine hawaamini. Yesu anaeleza jinsi Neno la Mungu lilivyo muhimu kwa watu ili waweze kuamini. Yesu anaeleza jinsi mali inavyowazuia watu wasipate imani.

### Swali la Matumizi

Kama kikundi kidogo au Jumuiya ya Umisheni, mnawezaje kuzidisha athari zenu nzuri katika jumuiya unayoishi?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Hatua ya Nne

# 04

## Ni wakati wa kuzidisha!

Katika Sehemu ya 17 ya Sinema ya *YESU* (JESUS film), Yesu anafundisha kuhusu kuzaa matunda. Wakati huu kikundi chako kidogo kitakuwa tayari kuamza tena na Hatua ya Kwanza ya kuanzisha jumuiya ingine mpya!

Watakuwa tayari wamejifunza kuhusu nguvu za Yesu juu ya ibilisi, nguvu zake juu ya hali asili, uwezo wake wa kuponya wagonjwa, kusamehe dhambi, sifa za mfuasi wa Yesu, na matarijio ya Yesu ya kuzaa matunda.

Huenda tayari umekwishamchagua mfuasi mkuu, Timotheo wako, ambaye ataweza kuongoza kundi hili jipya. Msaidie kufuata hatua 1-4 ili kuanzisha kundi jipya la kuzidisha!

Tunaomba kwamba Mungu akubariki unapomwamini Yeye kukutumia kama sehemu ya upanuzi wa Ufalme wake Mkuu!

KIKUNDI KIPYA KINACHOANZA KIRUDI KATIKA UKURASA WA KWANZA WA KITABU HIKI ILI KUANZA MCHAKATO UPYA!
WALIOBAKI KATIKA KUNDI HILI WAENDELEE NA SOMO LA 18 NA KUENDELEA!

# Sehemu ya 18: Mfano wa Taa (Luka 8:16-18)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Fikiria juu ya kile ambacho mwanga hufanya. Bila mwanga tusingeweza kufanya lolote baada ya jua kutua. Tungeishi kwa kuogopa kile kilicho gizani. Hatungeweza kuona tunakokwenda bila mwanga. Nuru haituonyeshi tu hatari zinazoweza kutokea, bali inaleta faraja tunapoweza kuwaona wapendwa wetu na mazingira yetu. Maisha yangekuwaje bila nuru? Fikiria ingekuwaje kuishi mahali penye giza kila wakati!

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Yesu mara nyingi hutumia mifano ya kawaida katika jumbe zake. Je, hii inatuambia nini kuhusu Yeye?
3. Unafikiri mfano wa nuru unahusianaje na watu kujua ukweli? Je, ni nani Yesu anazungumza juu yake anapoelezea juu ya nuru?
4. Unafikiri Yesu anamaanisha nini anaposema, “Hakuna lililofichwa ambalo halitafunuliwa.” Je, anarejea tukio gani hapa?
5. Ni kwa nini Mungu ahukumu watu? Unafikiri sababu ya jambo hili ni nini?
6. Je, inamaanisha nini anaposema, “Atapewa zaidi”? Je, hii inahusiana vipi na maisha ya Mkristo kabla ya yeye kwenda mbinguni?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, unaweza kumwambia Mungu nini kama ungesimama mbele zake leo na kujieleza jinsi ulivyoishi?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 19: Yesu Anatuliza Dhoruba (Luka 8:22-25)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Je, umewahi kuwa katika hali ya kutishiwa maisha? Kitu kama dhoruba, mafuriko, moto, na ajali ya gari, vita au ugonjwa mbaya? Ikiwa umewahi, shirikisha kikundi lako hadithi hiyo kwa kifupi na jinsi ilivyoathiri maisha yako.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, Unafikiri ina maana gani kwamba Yesu angeweza kulala nyuma ya mashua wakati dhoruba kali ilikuwa ikitokea baharini?
3. Je, ungejisikiaje kama ungekuwa ndani ya mashua wakati wa dhoruba? Je ni hisia gani unafikiri ungekuwa unapitia?
4. Je, Yesu anasema ni nini ambacho wanafunzi walikosa maishani mwao?
5. Je, hili linasema nini kuhusu Yesu kwamba angeweza kutuliza dhoruba kwa neno?
6. Je, kama wanafunzi kweli walikuwa na imani katika Yesu, unafikiri wangefanyaje wakati wa dhoruba hii?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Yesu anaonyesha kwamba Yeye ni mwanadamu kwa kulala usingizi wakati wa dhoruba, kwa kuwa alikuwa amechoka kutokana na huduma yote aliyokuwa amefanya. Hata hivyo, Yesu anathibitisha Yeye ni Masihi kwa kuweza kutuliza dhoruba. Yesu anatazamia wanafunzi walipaswa kujua kwamba angewatunza. Na pia alitarajia kuwa wanafunzi walipaswa kuwa na imani na kumwamini.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 20: Uponyaji wa Mwenye Pepo (Luka 8:26-39)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Moja ya wajibu wa kila Mkristo ni kuwaambia wengine kuhusu Yesu. Hii inaweza kufanywa kwa njia nyingi na katika mipangilio mingi tofauti. Yesu alifanya jambo hili kuwa sehemu ya Agizo Kuu aliposema, “Enendeni ulimwenguni mwote mkawafanye wanafunzi.” Sehemu ya kwanza ya kufanya mwanafunzi ni kumwambia mtu kuhusu Yesu. Katika hadithi hii Yesu kwa ujasiri anamkaribia mtu aliyeachwa na watu wengine. Anathibitisha Yeye ni Mwana wa Mungu kwa kuwa na mamlaka juu ya pepo.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Pepo walimwitaje Yesu? Je, hii inaonyesha nini kuhusu ujuzi wao wa Yesu ni nani?
3. Je, pepo walimwathirije mtu aliyekuwa amepagawa?
4. Unafikiri ni kwa nini pepo waliomba kutumwa kwa nguruwe? Hii inaweza kutwambia nini kuhusu mapepo?
5. Wale walioona jambo hilo likitukia walifanya nini? Unafikiri walifikiri nini kuhusu Yesu?
6. Mtu huyo alifanya nini baada ya mapepo kumwacha? Unafikiri alifikiria nini kuhusu Yesu? Yesu alimwambia afanye nini?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Unaogopa vitu gani? Je, Yesu anaweza kukusaidia vipi kushinda woga wako?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chako jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) ya mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 21: Yesu Analisha 5,000 (Luka 9:10-17)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Yesu alikuja Duniani kimsingi ili kuturudisha katika uhusiano na Mungu kwa kusamehe dhambi zetu. Hata hivyo, Yesu anajali pia mahitaji yetu ya kimwili. Hatatutimizia mahitaji yetu siku zote jinsi tunavyotamani, ili tujifunze kumwamini Yeye zaidi. Yesu anataka tutambue kwamba kila mmoja wetu anahitaji kuwasaidia wengine kimwili na kiroho. Katika habari hii Yesu aliwalisha wanafunzi wake kimuujiza na watu wengine 5,000!

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, wanafunzi walikuwa na wasiwasi juu ya swala gani ambalo walimletea Yesu?
3. Unafikiri Yesu alikuwa anajaribu kutimiza nini akiwajibu wanafunzi wake?
4. Je, jibu lao lilifunua nini kuhusu jinsi wanafunzi walivyokuwa wakiitazama hali hiyo?
5. 5Je, swala hili linasema nini kuhusu Yesu kwamba angeweza kuzidisha kiasi kidogo cha chakula na kulisha maelfu ya watu.
6. Unafikiri wanafunzi walijifunza nini kwa kuokota chakula cha ziada?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, wewe hufanya nini wakati mahitaji yako ni zaidi ya rasilmali ulizo nazo?

Kuwa na shida kunaweza kutufunza kumwamini Yesu tunapokuwa kwenye hali ngumu.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 22: Petro anatangaza kwamba Yesu ndiye Kristo (Luka 9:18-20)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Hatimaye kila mtu anapaswa kuamua nini cha kuamini kuhusu Yesu. Watu wengi hawafanyi maamuzi ya dhati lakini badala yake hufanya uamuzi kwa kukwepa. Wanaamua kutoamua juu Yake na kwendelea kuishi maisha yao bila kujali. Wengine husema kwa uwazi, "Ndiyo, nitamfuata" au, "Hapana, nadhani Yesu ni mtu mzuri lakini niko sahihi kuishi maisha yangu peke yangu." Katika kifungu hiki, ilimbidi Petro kufanya uamuzi huo kwa ajili yake mwenyewe.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, wadhani ni kwa jinsi gani mambo ambayo Petro aliona na kusikia yaliweza kumshawishi kumtangaza kwake Yesu ni nani?
3. Je, kwa nini Yesu alitumia muda mwingi kuomba? Je, hii inawezaje kuwa mfano bora kwa wafuasi wake?
4. Je, ukweli kwamba umati haukumjua Yesu alikuwa nani unasema nini juu yao?
5. Je, umati ulisema kwamba Yesu alikuwa nani?
6. Kwa nini unafikiri Petro alijua Yesu alikuwa nani na umati haukujua?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, watu wengine wameathiri vipi mtazamo wako kwa Yesu? Je, uliamuaje Yesu ni nani?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 23: Kugeuka Sura (Luka 9:28-36)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Kuna watu wengi ambao wana mawazo kuhusu maana ya maisha. Kuna dini nyingi sana. Kuna habari nyingi sana zinazopatikana za kusoma kuhusu jinsi ya kupata kusudi la maisha. Tunageukia wapi ili kujua tunachopaswa kuamini? Jibu kwa maswali makubwa ya maisha kwa kweli ni rahisi sana: Msikilize Yesu. Kwa nini? Kwa sababu ya kile alichosema, kwa sababu ya kile alichokifanya na hasa kwa sababu Yeye ndiye mtu pekee aliyewahi kufufuka kutoka kwa wafu. Yesu ndiye tunayepaswa kumsikiliza tunapokuwa na maswali kuhusu maisha.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Hapa tena tunamwona Yesu akiomba. Je, unafikiri Yesu alikuwa anaomba juu ya nini?
3. Je, inaashiria nini kuhusu Yesu kwamba sura yake ilibadilika? Neno gani limetumika kuelezea sura yake?
4. Kwa nini unafikiri Musa na Eliya walikuwa pamoja na Yesu? Walikuwa wanazungumza kuhusu nini na Yesu?
5. Je, Petro alijibuje alipomwona Yesu akiwa na Musa na Eliya? Je, unafikiri wewe ungelijibuje?
6. Unafikiri ni kwa nini Mungu aliwaelekeza wamsikilize Yesu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Ikiwa Yesu alihitaji kuomba mara kwa mara, je, tunahitaji nasi kuomba kwa kadiri gani?
Je, umeridhika na maisha yako ya maombi? Je, ungependa kutumia muda mwingi zaidi katika maombi?
Je, yapi ni baadhi ya mambo ambayo yanakuzuia kuomba zaidi?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 24: Yesu Anamponya Kijana kutokana na roho chafu (Luka 9:37-45)

Kutazama nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa masiha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi

Kila mtu ana kiwango fulani cha imani. Swali sio kama una imani bali ni nani mlengwa wa imani yako. Kila Mkristo yuko katika safari ya kiroho ya imani, safari inayoanza na mtu kuweka imani katika Yesu. Kila mtu yuko kwenye hatua tofauti katika safari yake ya kiroho pamoja na Yesu na ataonyesha kiwango tofauti cha imani. Imani yetu kamwe haitawahi kuwa kamilifu, lakini inaweza kuwa nyingi. Moja ya ombi letu linatakiwa kuwa, Bwana, niongezee imani!

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyoisimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Yesu alikuwa akizungumza na nani aliposema, “Enyi kizazi kisicho na imani na kilichopotoka”? Anawakosoa nini?
3. Kwa nini roho chafu amtendea huyo kijana hivyo? Je, hii inatuambia nini kuhusu asili na tabia ya Shetani na mapepo wake?
4. Inasema nini juu ya Yesu kwamba anaweza kukemea roho mara moja na kumponya kijana huyo?
5. Wale walioona muujiza huu walifanya nini?
6. Majibu yao yanatuonyesha waliamini nini kumhusu Yesu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, ni kitu gani kwenye maisha yako kinakusumbua zaidi kwa sasa?
Je, unadhani Yesu anawezaje kukusaidia katika hali hii?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Jizoeze kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 25: Sala ya Bwana (Luka 11:1-4)

Kutazama nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi — Jinsi Unavyoweza Kuomba kwa Ujasiri

Kumewahi kusemwa, “Sala ni mazungumzo kati ya watu wawili wanaopendana—Mungu na mwanadamu.” Kwa ufupi, maombi ni kuwasiliana na Mungu. Hata hivyo, maombi ni zaidi ya maneno. Ni moyo kujieleza kwa Mungu. Ni ujuzi ndani ya uhusiano zaidi ya shughuli. Kama mtoto wa Mungu, unaalikwa kuja kwa ujasiri mbele zake katika maombi.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Kwa nini unafikiri mmoja wa wanafunzi alimwomba Yesu awafundishe kusali baada ya Yesu kumaliza kuomba?
3. Yesu anasema tuelekeze maombi yetu kwa nani? Je, kwa nini jambo hili ni muhimu?
4. Yesu anaposema, “Ufalme wako uje,” anaonyesha nini kuhusu wakati ujao?
5. Yesu anamaanisha nini anapomwomba Mungu atupe “mkate wetu wa kila siku”? Je, unafikiri ni nini umuhimu wa neno “kila siku”?
6. Je unafikiri ni kwa nini Yesu anaunganisha kuomba kwetu msamaha kwa Mungu na utayari wetu wa kuwasamehe wengine wanaotukosea?
7. Kwa nini unafikiri wakati mwingine ni vigumu sisi kuwasamehe wale ambao wametuumiza au waliotukosea?
8. Je, Mungu anaweza kutusaidia jinsi gani wakati wa majaribu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Maombi ni fursa kwetu sisi kama Wakristo. Tunaomba ili kuwa na ushirika na Mungu. Tunaomba ili kueleza mahitaji na matamanio yetu kwa Mungu. Tunaomba kuleta wasiwasi na hofu zetu kwake. Tunamwomba Mungu awasaidie wale tunaowajali. Tunaomba kwa Mungu ili awasaidie wengine kuelewa injili na kuja kwa Kristo. Mungu anatuamuru tuombe daima. Tunaomba kwa Baba katika jina la Bwana Yesu Kristo kupitia huduma ya Roho Mtakatifu. Tunamwomba Mungu kwa kumwabudu, kukiri, kushukuru na kumsihi. Tunapokaa ndani yake, tunaweza kuomba kwa ujasiri.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chako jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 26: Kufundisha kuhusu Maombi na Imani (Luka 11:9-13; 12:22-30; 17:5-6)

Kutazama nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi - Jinsi Unavyoweza Kujazwa Roho Mtakatifu

Katika kufundisha juu ya swala la maombi na imani, Yesu anatumia jozi hizi za maneno: “Omba”/“utapewa,” “Tafuta”/“utaona,” “Bisha”/“utafunguliwa.” Anatoa hoja muhimu kuhusu nia ya Baba ya kutupa ujazo kamili wa Roho Mtakatifu, ikiwa tutaomba. Wanafunzi walipojazwa na Roho Mtakatifu, walipokea nguvu isiyo ya kawaida kutoka kwa Mungu ambayo iliwabadilisha kutoka kuwa watu waoga hadi mashahidi wa kung'aa kwa Kristo. Walitumiwa na Mungu kubadili historia. Na nguvu hizi hizi— nguvu za Roho Mtakatifu—zinapatikana kwako ili kukuwezesha kuishi maisha matakatifu na yenye matunda kwa ajili ya Yesu Kristo.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, Yesu anaweka masharti gani kuhusu jinsi atakavyojibu maombi? Kwa nini kunaweza kuwepo baadhi ya maombi ambayo Mungu huenda asiyajibu? Toa mfano.
3. Je, unafikiri Yesu anamaanisha nini anaposema, “Basi, ikiwa ninyi mlio waovu”? Kwa nini kwamba watu wanaweza kuwa wema na waovu?
4. Soma Waefeso 5:18 katika Biblia yako. Mungu anatupa amri gani katika kifungu hiki?
5. Kwa nini unafikiri itakuwa muhimu kwetu kuwa na nguvu za Roho Mtakatifu ndani yetu?
6. Nguvu za Roho Mtakatifu zinawezaje kuonekana katika maisha ya Mkristo?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Roho Mtakatifu ni Mungu Mwenyewe. Alikuja kuishi ndani yako mara tu ulipompokea Kristo kama Mwokozi wako. Roho Mtakatifu alikuja kumtukuza Kristo na kuwaongoza waamini katika kweli yote. Kujazwa na Roho Mtakatifu ni kujazwa na Kristo. Tunajazwa na Roho Mtakatifu kwa imani. Kwanza, kila mmoja wetu lazima atamani kuishi maisha ambayo yatampendeza Bwana. Pili, ni lazima tuwe tayari kuyasalimisha maisha yetu kabisa kwake. Tatu, ni lazima kuungama kila dhambi inayojulikana ambayo Mungu huleta kwenye kumbukumbu zetu. Kisha kwa imani, ni lazima tumwamini Mungu atujaze Roho wake Mtakatifu, na kutupa nguvu za kuishi maisha ambayo ametuwekea.

---

**Kutazama Mbele**

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chako jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 27: Ole Kwa Wale Wanaosababisha Wengine Watende Dhambi (Luka 17:1-4)

Kutazama nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi

Hii ni sehemu hii fupi sana, lakini ujumbe wake ni muhimu sana. Inashughulika na dhambi na uhusiano wetu na wengine. Yesu anasema kwamba jaribu hakika litakuja, lakini ole wake yule anayesababisha wengine kutenda dhambi. Fungua Biblia yako kwenye Luka 17:1-4 na usome mistari inayofuata maneno ya Yesu katika sehemu hii.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Yesu anamaanisha nini anaposema, “Majaribu ya dhambi hakika yatakuja”? Je, hii inatuambia nini kuhusu maisha yetu?
3. Je, Yesu anasema nini kuhusu wale wanaowaudhi wengine? Je, hii inakuambia nini kuhusu jinsi Yesu anavyothamini watu na mahusiano?
4. Je, unafikiri Yesu anazungumza juu ya nani anaposema, “wadogo hawa”? Kwa nini unafikiri jambo hilo ni muhimu?
5. Je, wewe na mimi tunawezaje “kumchukiza” mtu? Toa baadhi ya mifano.
6. Tunapaswa kuchukua hatua gani ikiwa ndugu yetu anatukosea?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, imekuwa vigumu kwako kuwasamehe wengine waliokukosea? Kwa nini jibu lako ni ndiyo, au kwa ni siyo? Je, ni baadhi ya mambo gani uliyojifunza kutokana na masomo haya ambayo yanaweza kukusaidia?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chako jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tulmejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

**Sehemu hii ya 28: haijawekwa.**

**Sehemu hii ni fupi na haina kifungu cha Biblia cha kujifunza.**

**Endelea na sehemu ya 29.**

# Sehemu ya 29: Yesu Anakaa na Wenye Dhambi (Luka 5:29-32)

Kutazama nyuma

## Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

## Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

## Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

## Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

## Utangulizi

Tuna tabia ya kutumia muda na watu ambao ni kama sisi. Mara nyingi, tunawaepuka watu walio tofauti na sisi, hasa ikiwa watu hao ni wale tunaowaona kuwa "watu wabaya." Huenda tusijue la kuwaambia. Huenda hatujui namna ya kufanya mambo karibu nao. Huenda tusitake hata kuonekana tukiwa nao au tunaweza tu kutojisikia vizuri kuwa karibu nao. Hata hivyo, Yesu hakuwahi kujisikia vibaya kwa njia yoyote kuwa karibu na watu "wenye dhambi." Kwa hakika, anaonekana kuwa alitumia muda mwingi katika kundi la wale wanaoonekana kuwa watu waliotengwa na jamii: watoza ushuru, wagonjwa, vipofu, watu wa mataifa ya kigeni, wenye ukoma na hata makahaba.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Kwa nini Mafarisayo walihoji Yesu kuwa alikula pamoja na "wenye dhambi"?
3. Unafikiri inamaanisha nini Yesu anaposema, "wale walio na afya njema"? Hapa anazungumzia nani?
4. Anarejelea nani anaposema, "walio wagonjwa"? Anamaanisha nini kutumia neno "wagonjwa"?
5. Unafikiri neno "toba" linamaanisha nini? Tumesikia wapi neno hili kabla? (Angalia nyuma kwenye Somo la 4 ikiwa muda unaruhusu).
6. Kwa nini Mafarisayo waliwaona wakusanya-kodi kuwa "watenda-dhambi"?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

## Swali la Matumizi

Je! ni kina nani baadhi ya watu katika utamaduni wako ambao wanaweza kuchukuliwa kuwa watu waliotengwa? (wasiofaa)?
Je, unapaswa kuwaonaje wale ambao utamaduni wako unawaona kuwa "wenye dhambi"?

---

Kutazama Mbele

## Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 30: Uponyaji siku ya Sabato (Luka 13:10-17)

Kutazama nyuma

## Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

## Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

## Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

## Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

## Utangulizi

Yesu alipendwa na watu, naye aliwapenda pia. Watu pekee ambao daima walionekana kutompenda Yesu walikuwa viongozi wa kidini wa Israeli. Mara nyingi Yesu alikuwa na maneno makali kwao, kwa sababu walijaribu kuwadhibiti watu kwa sheria na mapokeo waliyotunga. Yesu hakutaka kuwatawala watu; alitaka kuwaweka huru. Pia hakutaka pesa kutoka kwa watu, kama viongozi wa kidini walivyotaka, Yesu alitaka mioyo yao.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Mwanamke aliyeponywa alijibu vipi? Unafikiri alijisikiaje kuhusu Yesu baada ya kuponywa?
3. Mtawala wa sinagogi alimjibuje Yesu? Unafikiri yeye alifikiri nini kuhusu Yesu?
4. Yesu anamjibuje mkuu wa sinagogi? Je, mazungumzo yao na Yesu yalifunuaje moyo wa mtu huyo?
5. Unafiki ni nini? Unaweza kutoa mfano?
6. Kwa nini umati ulitambua kwamba Yesu alikuwa akifanya "mambo ya utukufu" na viongozi wa dini hawakufanya hivyo? Je, ukweli huu unasema nini kuhusu makundi hayo yote mawili?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

## Swali la Matumizi

Umejifunza nini kuhusu Yesu kutokana na somo hili?
Je wewe unalingana na nani zaidi, viongozi wa dini au makutano?

---

Kutazama Mbele

## Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 31: Mfano wa Msamaria Mwema (Luka 10:25-37)

Kutazama nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi — Jinsi Unavyoweza Kupenda kwa Imani

Upendo ndio kitu kikuu zaidi ulimwenguni—fursa kuu na uwezo mkuu unaojulikana kwa mwanadamu. Katika habari hii mwanasheria alisema ukweli aliposema tunapaswa kumpenda Mungu na jirani kama nafsi zetu. Lakini kisha akamuuliza Yesu, “Jirani yangu ni nani?” Yesu anajibu kwa kusimulia hadithi ambayo Msamaria (kundi la watu waliochukiwa na Wayahudi) ndiye mtu pekee anayemsaidia mtu aliye katika uhitaji mkubwa. Ni kwa uwezo wa Mungu pekee (nguvu anazotupa Yesu) tunaweza kuwapenda jirani zetu bila masharti, kama vile Mungu anavyotupenda.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Ni swali gani analoulizwa Yesu mwanzoni mwa hadithi hii?
3. Yesu anamjibuje mtu huyo? Je, hii inatuambia nini kuhusu umuhimu wa Bibilia?
4. Unafikiri nini kinafunuliwa kuhusu moyo wa mwanasheria kwa swali lake la pili alilomuuliza Yesu?
5. Ni watu gani ambao hawakumsaidia mtu aliyenyanganywa vitu vyake? Kwa nini unafikiri walishindwa kumsaidia mtu huyu aliyejeruhiwa?
6. Msamaria alionyeshaje kwamba “alimpenda jirani yake”? Upendo huu ulimgharimu nini Msamaria?
7. Je, unaweza kutengeneza orodha ya watu ambao ungependa kuwaonyesha upendo wiki hii? Kikundi chako kinawezaje kuonyesha upendo kwa wengine katika jamii yako?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati - Mambo matano ya kukumbuka kuhusu Upendo

1. Mungu anatupenda bila masharti.
2. Tumeagizwa kuwapenda wengine.
3. Hatuwezi kupenda kwa nguvu zetu wenyewe.
4. Tunaweza kupenda kwa upendo wa Mungu.
5. Tunapenda kwa imani, kama vile tulivyompokea Yesu kwa imani.

---

**Kutazama Mbele**

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.

# Sehemu ya 32: Uponyaji wa Bartimayo (Luka 18:35-43)

Kutazama nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi

Mambo yangekuwa vipi kama ungekuwa kipofu? Labda unamjua mtu ambaye ni kipofu. Wakati fulani ni lazima wawategemee wengine kwa mambo ambayo watu wanaoweza kuona wanayachukulia kawaida. Katika siku za Yesu, vipofu kwa kawaida walikuwa watu wa kuomba. Walipata msaada mdogo sana kutoka kwa mtu yeyote, na desturi, watu walidhania kwamba vipofu ni lazima walikuwa wamefanya dhambi na kuwa vipofu. Fikiria kwa muda jinsi maisha yako yangekuwa kama ungekuwa kipofu. Maisha yako yangewezaje kuwa tofauti?

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno y ake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Kipofu anafanya nini anaposikia kwamba Yesu anapita hapo? Je, anampa Yesu cheo gani alipopiga kelele? Kwa nini unafikiri jambo hilo linaweza kuwa muhimu?
3. Yesu anaamuru yule kipofu aletwe kwake. Je, unafikiri hili linafunua nini kuhusu moyo wa Yesu?
4. Yesu anamuuliza swali gani kipofu? Anajibuje?
5. Mwanamume huyo alionyeshaje shukrani na upendo wake kwa Yesu baada ya kuponywa?
6. Umati ulifanya nini? Unafikiri umati uliamini nini kuhusu Yesu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Kama Yesu angekuwa amesimama mbele yako sasa hivi, ungemwomba akufanyie nini?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Jizoeze kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tuliyojifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 33: Yesu na Zakayo (Luka 19:1-10)

Kutazama nyuma

## Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

## Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

## Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

## Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

Kutazama juu

## Utangulizi

Ukristo ndiyo dini pekee ambayo watu wanaweza kuokolewa bila kuupata kupitia juhudi zao wenyewe au matendo mema. Kila dini nyingine inahitaji aina fulani ya matendo ambayo watu lazima wafanye ili kupata wokovu. Lakini pia Ukristo una mahali pa matendo). Matendo huwa sehemu ya maisha ya Mkristo baada ya kuokolewa; si kabla. Kazi nzuri wanazofanya Wakristo ni matokeo ya maisha yao yaliyobadilika.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, unafikiri Zakayo aliamini nini kuhusu Yesu? Unafikiri kwa nini alipanda juu ya mti ili amwone Yesu?
3. Unafikiri kwa nini Yesu alijialika mwenyewe kwenye nyumba ya Zakayo?
4. Umati uliitikiaje kwa Yesu kusema anaenda nyumbani kwa Zakayo? Unafikiri ni kwa nini waliitikia kwa njia hiyo?
5. Zakayo anaonyeshaje kwamba amemwamini Yesu sasa? Ni mabadiliko gani anaonekana kufanya katika maisha yake?
6. Yesu anasema kusudi lake la kuja duniani ni nini? Je! Anatumia maneno gani kuelezea misheni yake?

## Swali la Matumizi

Ni kwa njia gani kumtumaini Yesu kumebadilisha mtazamo wako juu ya maisha?
Unaweza kushirikisha baadhi ya mifano ya mabadiliko hayo?

Kutazama Mbele

## Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chako jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 34: Yesu Anatabiri Kifo Chake na Ufufuo (Luka 18:31-34)

Kutazama nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi

Wakati watu maarufu wana wasifu (taarifa juu ya maisha yao) iliyoandikwa juu yao, mara nyingi taarifa kidogo sana husemwa juu ya kifo chao. Wasifu mwingi unaangazia wao walikuwa nani na walifanya nini ili kuwa maarufu. Yesu, hata hivyo, alikuja ili kufa. Huo ndio ulikuwa utume wake. Kwa hiyo, haipasi kutushangaza kwamba kila moja ya Injili (Vitabu vya Mathayo, Marko, Luka na Yohana) imeandika mengi kuhusu hali zinazozunguka kifo cha Yesu. Katika kifungu hiki Yesu, kwa mara nyingine tena anatabiri kifo na ufufuo wake ujao.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Hii ni mara ya tatu kwa Yesu kutabiri kifo chake kwa wanafunzi. Je, unafikiri ni kwa nini Yesu anarudia kuwaambia wanafunzi juu ya kile kitakachoenda kutokea kwake?
3. Unaelewa nini kutokana na ukweli kwamba Yesu alijua jinsi gani na lini atakufa kabla haijatokea?
4. Ikiwa Yesu alijua jinsi atakavyokufa, na Yeye ni Mwana wa Mungu, kwa nini hakuchukua hatua za kuepuka kifo?
5. Baada ya kifo chake, Yesu alipofufuka kutoka kwa wafu, jambo hilo linasema nini kuhusu Yesu?
6. Unafikiri ni kwa nini yale ambayo Yesu alikuwa akisema kuhusu kifo na ufufuo wake ujao ilifichwa kwa wanafunzi?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Yesu alijua kwamba atateseka na kufa ili kulipa adhabu ya dhambi zetu. Alikuwa tayari kabisa kufanya hivyo kwa sababu ya upendo wake kwetu. Je, ni baadhi ya njia gani unaweza kuweka mahitaji ya wengine mbele ya mahitaji yako mwenyewe?
Je, ni nani unayemjua kati ya marafiki au familia yako anayehitaji kuelewa kwa uwazi kuhusu Yesu ni nani na alichowafanyia? Unaweza kufanya nini wiki hii ili kuwasaidia kuelewa hili vyema?

---

**Kutazama Mbele**

### Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.

# Sehemu ya 35: Kuingia kwa Yesu kwa Ushindi (Luka 19:28-40)

Kutazama nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi

Mfalme huwa vipi? Ana uwezo, mamlaka, watu wanaomtumikia, na uwezo wa kufanya chochote anachotaka. Lakini ona jinsi Yesu alivyo tofauti akiwa mfalme! Anatanguliza mahitaji ya watu wake na kutafuta furaha na baraka zao juu ya vitu vyote vingine. Kwa sasa, Yesu anatawala katika mioyo ya wafuasi wake, na hatimaye, atatawala ufalme utakaodumu milele. Katika kifungu hiki, Yesu anatimiza unabii kutoka Zekaria 9:9. Someni mstari huo kwa sauti katika kikundi chenu.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri hadithi hii inatuonyesha nini kuhusu Yesu kwamba alijua hasa mahali ambapo punda alipokuwepo? Je, ungefikiria nini ikiwa ungekuwa mmiliki wa punda?
3. Kwa nini wanafunzi walifurahi na kumsifu Mungu kuhusu Yesu? Unafikiri wanafunzi hawa waliamini nini kuhusu Yesu?
4. Mafarisayo waliitikiaje tukio hilo? Kwa nini waliitikia jinsi walivyofanya? Kwa nini hawakufurahi pamoja na umati?
5. Yesu anamaanisha nini anapowaambia viongozi wa kidini kwamba ikiwa watu wangenyamaza, mawe yangepaza sauti ya kumsifu?
6. Katika utamaduni wao, kutandaza matawi ya mitende na nguo njiani mbele ya mtu ilikuwa heshima kubwa iliyotunzwa kama ishara ya heshima kwa wafalme. Je jambo hili laweza kutuambia nini kuhusu jinsi walivyokuwa wakimtendea Yesu?

### Swali la Matumizi

Je, wewe huwa na mwelekeo wa kuitikiaje unapomfikiria Yesu? Je, kweli unamtambua kuwa ni Bwana na Mfalme wako? Je, kuna maeneo yoyote ya maisha yako ambayo hujajisalimisha kikamilifu kwa Yesu? Ikiwa ndivyo, ni nini kinakuzuia kufanya hivyo?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 36: Yesu Analilia Yerusalemu (Luka 19:41-44)

Kutazama nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi

Inaweza kuwa vigumu sana kupata amani katika ulimwengu huu. Matakwa ya maisha, magumu tunayokabiliana nayo katika mahusiano yetu na wengine, na mateso tunayopata tunapoishi katika ulimwengu huu wenye dhambi na ulioanguka yanaweza kutunyang'anya amani tunayotamani. Katika kifungu hiki, Yesu anaomboleza ukweli kwamba taifa la Israeli (lililofananishwa hapa na jiji la Yerusalemu) halitapata amani kwa sababu wamemkataa.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri ni kwa nini Yesu analia anapoiona Yerusalemu? Kulia Kwake kunafunua nini kuhusu moyo wake kwa wanadamu?
3. Katika mst. 42 Yesu anasema Yerusalemu ingepata nini kama wangemwamini? Kwa nini hili ni muhimu?
4. Kutokuamini kwa Yerusalemu kulifanya mioyo yao kuwa migumu kwa mambo ya Mungu, kwa hiyo hawakuweza kumwona Yesu – Masihi – aliyekuwa mbele yao. Je, baadhi ya mambo ambayo yanaweza kusababisha mioyo yetu kuwa migumu ni yapi?
5. Unafikiri inamaanisha nini wewe kuwa na amani katika maisha yako? Ni baadhi ya njia gani ambazo watu hujaribu kupata amani maishani mwao?
6. Yesu anasema ni nini kinachokwenda kutokea kwa Yerusalemu? Kwa nini Yesu anasema hili litatokea?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, umewahi kupata mashaka au kutoamini katika maisha yako? Je, unaweza kutoa mfano wa hali hiyo?
Je, baadhi ya mambo ambayo Wakristo wanaweza kufanya ili kusaidia imani yao ikue kwa nguvu ni yapi?
Je, unaweza kushiriki baadhi ya mifano kutoka kwa maisha yako mwenyewe?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chako jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 37: Yesu Awafukuza Wanaobadili Pesa (Luka 19:45-48)

Kutazama nyuma

## Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

## Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

## Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

## Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

## Utangulizi

Katika Maandiko, Yesu alizungumza kuhusu fedha mara nyingi zaidi kuliko jambo lingine lolote. Huenda hilo ni kwa sababu Yesu alijua kwamba pesa ni jambo la lazima kwa maisha yetu ya kila siku. Lakini pia ni kiashirio bora zaidi cha kile ambacho tunatilia umuhimu zaidi maishani. Ni bahati mbaya kwamba dini na pesa ni mambo yamekuwa na historia ngumu. Ingawa hakuna ubaya wa kimaadili na fedha yenyewe, dini nyingi hujaribu kupata pesa nyingi iwezekanavyo kutoka kwa wafuasi wao. Inasikitisha pia kwamba viongozi wengi wa kidini mara nyingi hutumia pesa wanazokusanya kutoka kwa wafuasi wao kuishi maisha ya anasa. Yesu anatuonyesha katika habari hii jinsi anavyohisi kuhusu wale wanaotafuta kupata pesa kutokana na dini. Hapa anakasirika kwamba wanawadhulumu watu katika Hekalu, ambalo ni nyumba ya Mungu.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, habari hii inaonyesha nini kuhusu Yesu kwamba aliwakasirikia wale waliokuwa wanafanya biashara Hekaluni?
3. Yesu anasema Hekalu linapaswa kuwa nini? Unafikiri hii inamaanisha nini?
4. Unadhani kwa nini Yesu alipinga watu kuuza matoleo Hekaluni?
5. Je, Yesu anawaelezaje wale waliokuwa wakiuza matoleo Hekaluni? Unafikiri ni kwa nini aliwaelezea hivyo?
6. Unafikiri ni kwa nini viongozi wa kidini walitaka kumuua Yesu? Kwa nini walikuwa wanasumbuka kupata njia ya kufanya hivyo?

## Swali la Matumizi

Je, kuna maeneo yoyote ya maisha yako ambapo unaweza kuwa unamnyanyasa mtu mwingine?
Ikiwa ndivyo, unahitaji kufanya nini ili kubadilisha hali hiyo?
Ni baadhi ya mambo gani tunaweza kufanya ili kutusaidia kuweka maombi kuwa jambo la kwanza katika uhusiano wetu na Kristo?

---

**Kutazama Mbele**

## Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 38: Sadaka ya Mjane (Luka 21:1-4)

Kutazama nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi - Jinsi Unavyoweza Kupitia Matukio ya Utoaji

Mungu anawapenda wajane na yatima. Katika siku za Yesu, kwa kawaida wajane walikuwa miongoni mwa watu maskini zaidi. Katika hadithi hii, tunaona mjane akitoa kila kitu alichokuwa nacho kama sadaka kwa Mungu! Alionyesha dhana inayoitwa usimamizi. Hii ni imani kwamba kila kitu tunachomiliki ni cha Mungu na sisi ni "wasimamizi" wa mali za Mungu. Maisha yako pia yanaweza kuonyesha usimamizi huo. Utoaji kwa imani ni jambo ambalo kwa Mungu ni fursa yenye kusisimua. Unapompa heshima Mungu kupitia kujitoa kwako na kuwa mtiifu kwa usimamizi, Yeye anakumiminia furaha. Anageuza utoaji wako kuwa tukio la kufurahisha katika maisha ya Kikristo.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, unadhani ni rahisi kwa matajiri kutoa pesa kuliko masikini?
3. Kwa nini mjane alitoa kila kitu alichokuwa nacho? Je, hii inatuambia nini kuhusu imani yake binafsi kwa Mungu?
4. Unafikiri ni kwa nini Yesu alitumia muda mwingi kuzungumza kuhusu pesa na matajiri?
5. Shirikishi njia ambayo Shetani anaweza kukujaribu utoe kidogo. Sema kwa uwazi. Je, unawezaje kushinda jaribu hili katika siku zijazo?
6. Katika kikundi chenu, orodhesha njia kadhaa ambazo mnaweza kushiriki utele wenu pamoja na wengine kwa njia ya utoaji wa vitu na kwa njia zingine.
7. Je, unafikiri Yesu anatarajia hata maskini watoe pesa kwa kanisa?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Vyote tulivyo navyo, tunavimiliki kwa sababu Mungu ametupatia. Kwa hiyo vyote tulivyo navyo ni vyake. Kazi yetu kama "wasimamizi waaminifu" ni kusimamia baraka hizo ili kuleta utukufu wa hali ya juu kwa jina lake. Tunapojitolea kwa hiari sisi wenyewe, na mali zetu, tunaonyesha kwa njia dhahiri utegemezi wetu wa kiroho kwa Kristo. Mungu anajua mahitaji yetu na anataka tumtegemee ili atupatie mahitaji yetu. Mtume Paulo aliwaandikia hivi Wakristo wa Filipi: "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake ndani ya Kristo Yesu" (Wafilipi 4:19). Kwa imani, Mungu hutupatia mahitaji yetu yote tunapomwamini na tunapotoa kwa ukarimu.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chemu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 39: Anasi Anatilia shaka Mamlaka ya Yesu (Luka 20:1-8)

Kutazama nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

Kutazama juu

### Utangulizi

Katika ulimwengu wetu leo, watu wanaweza kusema jambo bila kujua kwamba ni kweli au hata kuamini kwamba ni kweli. Dini hufanya vivyo hivyo kwa kufundisha mambo ambayo hayawezi kuthibitishwa kuwa kweli. Ikiwa unaamini, kwa mfano, kwamba ng'ombe ni takatifu, unajuaje hilo kuwa kweli? Imani hiyo inatoka wapi? Ikiwa imetoka katika kitabu, unajuaje kwamba kitabu hicho kinaaminika? Yesu ni wa pekee kati ya viongozi wa kidini kwa sababu maneno yake yalithibitika kuwa ya kweli kupitia tabia yake, mafundisho yake, miujiza yake, na ufufuo wake kutoka kwa wafu.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, unaweza kuelezaje mtazamo wa viongozi wa kidini walipokuja kumwuliza Yesu maswali? Je, jambo hili linatuambia nini kuhusu mioyo yao?
3. Walimuuliza Yesu swali gani? Unafikiri ni kwa nini walimuuliza hivyo?
4. Yesu aliwajibu viongozi wa kidini kwa swali. Aliwauliza swali gani? Unafikiri ni kwa nini alichagua kuwajibu hivyo?
5. Kwa nini viongozi wa kidini hawakuamini kwamba Yohana Mbatizaji alitumwa na Mungu? Unafikiri hii inaonyesha nini kuhusu mioyo yao?
6. Unafikiri Yesu alipata wapi mamlaka ya kufanya miujiza na kufundisha? Je, hili linasema nini juu Yake?

### Swali la Matumizi

Je, unaweza kufikiria sehemu zozote za maisha yako ambazo hujajitoa kikamilifu kwa Yesu? Ikiwa ndivyo, ni nini kinachoweza kukushawishi kufanya hivyo?

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 40: Mfano wa Shamba la Mizabibu na Wapangaji (Luka 20:9-19)

Kutazama nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi

Kama taifa, Israeli walikuwa watu waliochaguliwa na Mungu. Yesu alipokuja kama Masihi, walimsikiliza akifundisha, walitazama tabia yake, na walimwona akifanya miujiza. Walimsifu kama Mfalme wao alipoingia Yerusalemu akiwa amempanda punda, lakini baada ya siku chache tu, viongozi wao wa kidini waliwaongoza watu kumkataa. Akijua hilo litatokea, katika sehemu hii, Yesu anawapa watu hao hadithi kuhusu mmiliki na wakulima wa shamba la mizabibu (bustani ambamo zabibu hupandwa). Kupitia hadithi hii, Yesu anaonya kuhusu matokeo ya kumkataa.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri nini maana ya mfano huu? Yesu anazungumza juu ya nani?
3. Yesu anasema nini kitatokea kwa wale wanaomuua mwana wa mwenye shamba?
4. Yesu mara nyingi ananukuu vifungu vya Agano la Kale ambavyo vilimtaja Masihi. Unafikiri kwa nini anafanya hivi? Je, hii inatuambia nini kuhusu Yesu?
5. Unafikiri Yesu anarejelea nini anaposema kwamba jiwe lililokataliwa linageuka kuwa jiwe kuu kuliko yote?
6. Soma Luka 20:19. Je, viongozi wa Kiyahudi waliitikiaje jambo hili? Ni nini kiliwazuia kufanya walichotaka kufanya?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Yesu alipata kukataliwa na viongozi wa Kiyahudi. Je, wewe hukabilianaje na hisia za kukataliwa? Yesu anaweza kukusaidiaje unapohisi kukataliwa?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 41: Kulipa Kodi kwa Kaisari (Luka 20:20-26)

Kutazama nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama juu

### Utangulizi

Wakati wa huduma ya Yesu, taifa la Israeli lilitawaliwa na Warumi. Walikuwa na gavana mwenye jukumu la kudumisha utulivu na kukusanya kodi lakini waliwaruhusu Wayahudi wawe na mfalme wao wa kusaidia kusimamia nchi (Mfalme Herode alikuwa mfalme wa namna hiyo). Wayahudi walichukia kulipa kodi kwa Warumi kwa sababu Warumi hawakuwa Wayahudi (walikuwa "Wamataifa", maana yake, "wasio Wayahudi"), na kwa sababu Warumi walitumia kodi zilizolipwa na wayahudi ili kuwaweka chini ya mamlaka yao.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, ni njia gani mpya ambayo viongozi wa Kiyahudi wanatumia hapa kujaribu kumtega Yesu? Je, hii inaonyesha nini kuhusu shauku yao ya kumuua Yesu?
3. Tunamwitaje mtu anayejifanya kuwa kitu fulani na kumbe sivyo? Je, unadhani hili ni jambo la kawaida miongoni mwa watu kila mahali? Kama ni hivyo, Kwa nini huwa hivyo?
4. Yesu alijua kwamba viongozi wa kidini walikuwa wakijaribu kumtega. Je, hii inasema nini juu yake kwamba hakutishwa nao?
5. Yesu anajibuje swali lao? Unafikiri anamaanisha nini kwa swali ambalo naye anawauliza?
6. Unafikiri ni kwa nini viongozi wa kidini hawakuweza kumtega Yesu kwa maswali?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, kuna maeneo yoyote ya maisha yako ambapo unajifanya kuwa kitu ambacho hauko hivyo? Ikiwa ndivyo, ungama hayo kwa Mungu sasa hivi. Yeye anatamani tuwe waaminifu kabisa kujihusu sisi wenyewe.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 42: Karamu ya Mwisho (Luka 22:14-23)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Pasaka ilikuwa sikukuu ya Wayahudi iliyoanzishwa na Mungu katika Agano la Kale. Lilikuwa ni tukio takatifu kwa Wayahudi ambalo liliadhimishwa wakati ambapo Mungu aliwaepusha na pigo la kifo cha kimwili na kuwatoa katika utumwa huko Misri. Karamu ya Mwisho ilileta maadhimisho ya Agano la Kale ya sikukuu ya Pasaka kwenye utimilifu wake. Wakati wa Karamu ya Mwisho na wanafunzi wake, Yesu alichukua ishara mbili zinazohusiana na Pasaka na kuzipa maana mpya. Mkate na divai hutusaidia kukumbuka dhabihu yake, ambayo hutuokoa kutoka kwenye kifo cha kiroho na kutukomboa kutoka kwenye utumwa wa kiroho.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri ni kwa nini Yesu alitaka kushiriki chakula cha mwisho pamoja na wanafunzi 12?
3. Mara mbili katika hadithi hii Yesu anataja "ufalme wa Mungu." Unafikiri anarejea nini hapa?
4. Mkate unawakilisha nini? Divai inawakilisha nini? Je, yote mawili yanarejea tukio gani?
5. Yesu anawaambia wanafunzi wafanye nini wakati ujao watakaposhiriki mkate na kunywa divai?
6. Yesu anasema mmoja wa wanafunzi atamfanyia nini? Je, unafikiri hili lilikuwa jambo ngumu kwa Yesu kuzungumzia kwa kiwango gani?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, ni mara ngapi wewe huchukua muda kutafakari binafsi na kukumbuka kifo cha Kristo?
Je, umewahi kusalitiwa na mtu? Je, alikufanya ujihisije?
Je, unafikiri Yesu alijihisi vivyo hivyo?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 43: Mafundisho ya Chumba cha Juu (Luka 22:26-38)

Kutazama Nyuma

## Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

## Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

## Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

## Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

## Utangulizi

Hisia za kawaida za kila mtu ni kutaka kuwa wa kwanza; hakuna anayetaka kuwa wa mwisho. Yesu, hata hivyo, anageuza aina hii ya fikra. Yesu anasema kwamba ukitaka kuwa wa kwanza, lazima uwatangulize wengine. Watu wengi wanataka kuwa viongozi, lakini ni watu wachache wanaotaka kutumika. Yesu pia anabadili hili tena na kusema kwamba ikiwa unataka kuwa kiongozi halisi, lazima ujifunze kuwatumikia wengine. Yesu alikuwa mfano wa mambo haya hasa. Aliendelea kuwatanguliza wengine na akawa mtumishi nambari moja kwa kuyatoa maisha yake kwa ajili yetu ili sisi tupate kuokolewa.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Ni kwa namna gani maisha ya Yesu yanakuwa kielelezo cha mtu aliyekuwa kiongozi mtumishi? Ni yapi baadhi ya mifano kutoka katika maisha yake?
3. Je, unafikiri ni jambo la kupingana mtu kuwa kiongozi mtumishi wakati mmoja? Je, unawezaje kuonekana kuwa kiongozi na mtumishi wakati mmoja?
4. Kwa nini unafikiri Yesu alimwambia Petro kwamba Shetani angempepeta?
5. Petro anaitikiaje onyo la Yesu? Kwamba yuko tayari kwenda gerezani au kufa kwa ajili ya Yesu. Je, unafikiri Petro alimaanisha kile alichosema akimjibu Yesu?
6. Ni kwa njia gani Yesu alikuwa akijaribu kuwatayarisha wanafunzi W wake hapa kwa ajili ya umisheni wao baada ya kufufuka kwake?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

## Swali la Matumizi

Ni zipi baadhi ya njia mahususi ambazo unaweza kuwatumikia wengine unapofuata mfano wa Yesu?

---

Kutazama Mbele

## Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 44: Yesu Asalitiwa na Kukamatwa (Luka 22:47-53)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Maisha ya Yesu kwa hakika yanahusu kifo chake. Kwa kila mtu mwingine, “maisha” yao yanajumuisha kila kitu ambacho wamefanya hadi kufa kwao. Kifo ni tukio la mwisho kutokea kwa watu na hutazamwa kwa huzuni kwa sababu watu tunaowapenda wamechukuliwa kutoka kwetu. Lakini kwa Yesu, kifo chake kilikuwa ndilo tukio muhimu zaidi katika maisha yake. Kifo cha Yesu kilifanya iwezekane kwa watu kuwa waliokubalika na Mungu kwa kumwamini.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri ni nini husababisha watu kuwasaliti wengine wanaowajua?
3. Yesu anamwambia nini Yuda? Unafikiri maneno Yake yanasema nini kuhusu uhusiano Wake na Yuda?
4. Je, wanafunzi wanafanyaje wanapoona kwamba Yesu anakaribia kukamatwa?
5. Yesu anatumia maneno gani kuonyesha kwamba yuko tayari kukamatwa?
6. Unafikiri ni kwa nini viongozi wa kidini walikuja usiku ili kumkamata Yesu? Unafikiri ni kwa nini Yesu anatumia maneno “mamlaka ya giza” hapa?

### Swali Matumizi

Yuda alimsaliti Yesu kwa ajili ya pesa. Je, kuna kiasi chochote cha pesa ambacho kinaweza kukufanya umsaliti rafikiyo?
Je, kuna mambo yoyote katika maisha yako ambayo unajaribiwa kuvichukulia kuwa vya maana zaidi kuliko Yesu?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 45: Petro Amkana Yesu (Luka 22:54-62)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Je, umewahi kufanya jambo ambalo unajutia? Je, ilikufanya ujisikieje? Je! ulikuwa na hisia za aibu, hatia, au labda ulijawa na majuto? Je, umeweka ahadi kwa mtu ambaye umeshindwa kutimiza? Je hilo lilikufanya ujisikieje? Katika hali hizo mbili, mtu mwingine alifikiria nini kukuhusu? Hadithi hii inachunguza mambo hayo yote mawili katika maisha ya Petro: kumkana kwake Yesu, na kushindwa kwake kutimiza ahadi yake.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri ni kwa nini Petro anakana kumjua Yesu?
3. Unafikiri kukana kwake kunaweza kutufundisha nini kutuhusu sisi wenyewe... mioyo yetu, hisia, na nia zetu?
4. Yesu alikuwa ametabiri kwamba Petro atamkana mara tatu. Je, hili linatuambia nini kuhusu Yesu?
5. Je tunajifunza nini kuhusu Yesu kwamba hakumkataa Petro kwa sababu ya kumkana kwake? Je, tunajifunza nini kwa ukweli kwamba hatimaye Petro alikuwa kiongozi mkuu katika kanisa la kwanza?
6. Fikiri nyuma katika somo la Sehemu ya 14 kuhusu "Kupumua Kiroho." Je, tunaweza kutumia mafundisho hayo vipi katika hali hii ya Petro kwenye somo hili?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Fikiria juu ya kitu kibaya sana ambacho umewahi kufanya. Je, unadhani Yesu angekusamehe kwa yale uliyofanya? Ikiwa ndivyo, kwa nini? Ikiwa sivyo, kwa nini?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 46 Yesu Anadhihakiwa na Kuhojiwa (Luka 22:63-71)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Sehemu hii ya Luka inaanza wakati wa kufedheheshwa kwa Yesu mikononi mwa Warumi na viongozi wa Wayahudi. Ingawa Yesu angeweza kuita umati mkubwa wa malaika kumwokoa na kumlinda, Yeye anajisalimisha kutendewa hivyo kwa sababu hii ilikuwa ni sehemu ya mpango wa Mungu kuwakomboa wanadamu.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. 2Unafikiri ni kwa nini Yesu hakufanya lolote ili kukomesha ukatili aliokuwa akitendewa?
3. Walinzi walimtendeaje Yesu? Unafikiri ni kwa nini walimtendea hivyo?
4. Je, unafikiri viongozi wa kidini walitaka kweli kujua ikiwa Yesu ndiye Masihi? Kwa nini wamuulize swali hili?
5. Majina ya vyeo kadhaa yametumika katika kifungu hiki kumwelezea Yesu. Je unafikiri kila moja ya hayo yanasema nini juu yake?
6. Mwishoni mwa sehemu hii ya sinema, viongozi wa kidini wanamwuliza Yesu swali moja la mwisho. Je, Yesu anawajibuje? Unafikiri hii inasema nini kumhusu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Fikiria juu ya wakati katika maisha yako ambapo ulipata mateso. Uliitikiaje jambo hilo? Je, una mwelekeo gani wa kukabiliana na mateso?
Je, unaweza toa mifano yoyote ya jinsi Mungu alivyoleta kitu kizuri kutoka kwa mateso ambayo umeyapitia?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 47: Yesu Analetwa kwa Pilato (Luka 23:1-5)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Ukristo siyo habari ya siasa. Hata hivyo, Wakristo wengi ulimwenguni pote wanaamini kwamba vyama fulani vya kisiasa ndivyo vinavyostahili kuungwa mkono na Wakristo kuliko vingine. Kwa karne nyingi watu wamejaribu kumtumia Yesu ili kuunga mkono misimamo yao kuhusu mambo mbalimbali ya kisiasa. Hata hivyo Yesu hakuja kwa ajili ya manufaa ya kisiasa. Badala yake, alikuja kutafuta na kuokoa waliopotea (tazama Luka 19:10).

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Kwa nini viongozi wa kidini walilazimika kumpeleka Yesu kwa Pilato? Walimshutumu Yesu kwa kufanya nini?
3. Je, Yesu alidai kuwa mfalme kwa maana ya kisiasa? Unafikiri ni kwa nini viongozi wa kidini walimshtaki Yesu kwa Pilato kuhusu jambo hili?
4. Yesu anajibuje anapoulizwa kama yeye ni Mwana wa Mungu? Kwa nini unafikiri anajibu hivyo? Katikati ya sehemu hii, Pilato alifikia hitimisho gani kumhusu Yesu? Viongozi wa Kiyahudi wanajibu vipi kwa hitimisho hilo?
5. Unafikiri ni kwa nini Pilato anaamua kumpeleka Yesu kwa Herode? Je, hii inafunua nini kuhusu tabia ya Pilato?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Yesu anatamani kutawala maishani mwetu. Ikiwa wewe ni mkweli, je unamruhusu kwa ukamilifu kiasi gani ayaongoze maisha yako? Je, tunawezaje kuhimizana kuyasalimisha maisha yetu zaidi kwa Kristo?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 48: Yesu Analetwa kwa Herode (Luka 23:6-12)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Herode alikuwa anakaa Yerusalemu kwa sababu ulikuwa wakati wa sherehe ya Pasaka. Alikuwa alikulia. Herode alitawala tu kwa ruhusa ya Warumi. Baada ya kifo na ufufuo wa Yesu, Herode angekuwa mnyanyasaji mkubwa wa Wakristo na hatimaye angemuua mtume Yakobo. Hadi Pilato alipomtuma Yesu kwake, Herode alikuwa bado hajaonana na Yesu, ingawa inaonekana alikuwa amesikia habari zake. Herode alikuwa mtu mwenye kiburi ambaye hatimaye Mungu alimuua alipokuwa akipokea ibada ya watu (Ona Matendo 12:21-23).

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Kwa nini Herode alitaka kumwona Yesu? Herode alitaka Yesu amfanyie nini?
3. Kwa nini wadhani kwamba watu fulani wanapendelea tu kukutana na Yesu ili awafanyie jambo la kimuujiza? Hilo linafunua nini kuhusu mioyo yao?
4. Unafikiri ni kwa nini Yesu hakumjibu Herode?
5. Herode alifanya nini wakati Yesu hakumjibu?
6. Unafikiri ni kwa nini Herode alimrudisha Yesu kwa Pilato?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Kwa nini wewe unamfuata Yesu? Je, kweli ni kwa sababu Yeye ni Bwana na anastahili utukufu na heshima zote? Au ni kwa sababu unataka akufanyie jambo fulani?
Je, umewahi kujikuta unatafuta kibali cha wengine badala ya kutaka kumpendeza Mungu? Je, unaweza kushiriki mifano yoyote?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 49: Yesu Anahukumiwa (Luka 23:13-25)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Wakati fulani tunaweza kupatana na shinikizo kutoka kwa watu wanaotuzunguka ili tutende kwa njia fulani. Shinikizo hilo linaweza kuathiri nia yetu ya kufanya yale tunayoamini kuwa ni sawa, kwa kuogopa wengine watawazaje. Hofu hiyo inaweza kutufanya tufanye mambo ambayo tusingepaswa kufanya au inaweza kutufanya tuache kufanya mambo ambayo tunapaswa kufanya. Inaonekana Pilato alitenda kwa woga kwa jinsi alivyomtendea Yesu. Luka 23:20 inasema kwamba Pilato alitaka kumwachilia Yesu, lakini alikubali matakwa ya umati walipoongeza madai yao.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, hukumu ya Pilato na Herode juu ya hatia ya Yesu ilikuwa ipi? Unafikiri waliegemeza mahitimisho yao juu ya nini?
3. Kwa nini Herode au Pilato hawakuamini mashtaka dhidi ya Yesu yaliyoletwa na Viongozi wa Kiyahudi? Unafikiri hii inatuambia nini kuhusu viongozi wa Kiyahudi?
4. Kwa nini Pilato alitoa uhuru wa Baraba kwa viongozi wa Kiyahudi na watu?
5. Pilato alitaka kumwachilia Yesu, lakini hakufanya hivyo. Ni nini kilimshawishi kukubali ombi la kumsulubisha Yesu? Unafikiri Pilato alikuwa ana hisia gani?
6. Kwa nini Yesu hakufanya lolote kumzuia Pilato au viongozi wa Wayahudi? (Tazama Mathayo 26:52-54)

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Unafikiri hofu hukuathirije? Je, unaweza kufikiria mfano wa kushirikisha hapa?
Je, wewe huwa unakabiliana vipi na hofu zako? Unafikiri Mungu angetamani ufanye nini juu ya hofu zako?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 50: Yesu Abeba Msalaba Wake (Luka 23:26-31)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujiuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidiwa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Katika sehemu hii, Yesu anabeba msalaba ambao atakufa juu yake hivi karibuni. Luka, ambaye ndiye mwaandishi mwanadamu wa kitabu hiki cha Biblia, bila shaka alitaka kukazia mlinganisho wa Yesu kutembea njiani katikati ya makutano kwenye njia ya kuelekea kifo chake na ile ya "kuingia kwake kwa ushindi" Yerusalemu siku chache tu zilizopita.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri kwa nini Yesu hakuweza kubeba msalaba wake mwenyewe njia nzima? Je, hii inaweza kusema nini kuhusu alivyotendewa na Warumi?
3. Simoni wa Kirene anatambulika kama mtu aliyelazimishwa kubeba msalaba wa Yesu wakati ule Yesu alipokuwa hawezi. Je unadhani Simon anaweza kuwa alihisi vipi alipokuwa anaubeba msalaba wa Yesu?
4. Wanawake waliokuwa wakimtazama Yesu walifanya nini? Je, unafikiri walikuwa na hisia za aina gani?
5. Unafikiri kwa nini Yesu anawaambia wanawake wasimlilie bali wajililie wenyewe?
6. Ni kwa njia gani unaona upendo wa Kristo ukionyeshwa katika habari hii?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Nini maoni yako - Je, ni rahisi kwako kukabiliana na mateso ya kimwili au mateso makubwa ya kihisia? Tafadhali elezea.
Katika kifungu kingine cha Biblia, huyu Simoni Mkirene anatambulika kama "baba yao Iskanda na Rufo", ambaye inaonekana kuashiria kwamba kanisa la kwanza liliwafahamu. Wanatheolojia wengi wangesema hii inamaanisha kwamba lazima baadaye walifanyika kuwa Wakristo. Je, kujitolea kwako kumfuata Yesu kumeathiri vipi familia yako?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 51-54: Yesu Anasulubishwa (Luka 23:32-43)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana Sisi kwa Sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

*Somo hili linatumia sehemu ya Sinema ya Yesu (*JESUS* film) ya wakati Yesu Anasulubiwa, Askari Wanapiga Kura kwa ajili ya Nguo za Yesu, Anwani Iliyowekwa Msalabani, pamoja na Wahalifu Waliosulubishwa*

### Utangulizi

Msamaha unaweza kuwa mgumu. Tunapoumizwa na mtu, tunaweza kupata maumivu, hasara, hasira, na wakati fulani, uchungu wa moyo. Mwitikio wa asili ya kuumizwa ni kutaka kulipiza kisasi. Hata hivyo akiwa msalabani, Yesu anawasamehe wale waliomweka pale. Katika maisha yetu, kuwasamehe wale ambao wametuumiza kwa kweli hutuweka huru. Msamaha husaidia kurudisha kwetu tena uwezo ambao tumewapa wengine kutudhoofisha vibaya na pia hutuletea amani na Mungu. Na tufuate mfano wa Yesu!

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Maneno ya kwanza ya Yesu kutoka msalabani yanahusisha msamaha. Je, unadhani Yesu alikuwa anawahusisha nani hapa? Je, hii inasema nini kuhusu upendo wa Kristo?
3. Watu wanaposema, "Aliokoa wengine, na ajiokoe mwenyewe," unafikiri wanamaanisha nini? Je, unafikiri watu wangemwamini Yesu kama angeshuka kutoka msalabani? Kwa nini waonelea hivyo?
4. Unafikiri mhalifu anamaanisha nini alipomwomba Yesu amkumbuke wakati akija kama Mfalme?
5. Ni kwa jinsi gani ujuzi huo wa mhalifu anayeonyesha imani katika Yesu ni mfano wa jinsi watu wote wanavyomjia Yesu?
6. Wale waliokuwa wakitazama walielewa kwamba Yesu alidai kuwa ndiye Masihi. Unafikiri walikuwa wanafikiria nini walipomwona msalabani?

### Swali la Matumizi

Je, ni vigumu kwako kusamehe watu wale wengine? Ni aina gani za makosa ni ngumu kwako kusamehe? Mfano wa Yesu wa kusamehe unaweza kukusaidiaje?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha hadithi ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.

# Sehemu ya 55: Kifo cha Yesu (Luka 23:44-49)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Katika Agano la Kale, taifa la Israeli lilimwendea Mungu kupitia kwa Hekalu. Hekaluni ndipo walipoleta dhabihu zao na kumwabudu Mungu pamoja. Mara moja kwa mwaka, "Kuhani Mkuu" (kuhani aliyekuwa juu ya wengine wote) alileta dhabihu maalum katika chumba cha ndani cha Hekalu kinachoitwa "Patakatifu pa Patakatifu." Dhabihu hii ilikuwa ni ya "kulipia" (kufunika) dhambi za watu. Patakatifu pa Patakatifu palitenganishwa na sehemu nyingine ya Hekalu kwa pazia kubwa. Katika sehemu ya leo, tunaona kwamba pazia hili lilipasuka Yesu alipokufa. Hilo lilionyesha kwamba njia ya kumfikia Mungu sasa ingekuwa ni kupitia kifo cha Yesu tu, sio kwa kupitia dhabihu iliyoletwa na kuhani.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Giza lilitanda juu ya nchi kwa muda wa saa tatu kabla ya Yesu kufa. Unafikiri giza hilo liliwakilisha nini?
3. Unafikiri Yesu alikuwa anaonyesha nini aliposema, "Baba mikononi Mwako naiweka roho yangu"?
4. Watu waliokuwa wakimtazama Yesu waliitikiaje tukio hilo?
5. Je, akida wa jeshi aliyekuwa akimtazama Yesu akifa aliitikiaje tukio hilo? Je, unafikiri alimwamini Yesu?
6. Kwa nini akida akiri kwamba Yesu alikuwa "mtu mwenye haki" wakati viongozi wa Kiyahudi walimkataa? je, unafikiri tunaweza kujifunza nini kutokana na jambo hili?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Yesu anaonyesha kiwango kikubwa cha imani yake kwa Mungu katika kufa msalabani. Kumtumaini kwake Mungu hivi kunawezaje kuwa kielelezo kwetu?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 56: Kuzikwa kwa Yesu (Luka 23:50-56)

Kutazama Nyuma

## Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

## Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

## Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

## Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

## Utangulizi

Baada ya Yesu kufa, mwanamume anayeitwa Yusufu aliendа kwa Pilato kuuomba mwili wa Yesu. Alikuwa mshiriki wa baraza lile lile la Kiyahudi lililomhukumu Yesu, lakini hakuwa amekubaliana na uamuzi wao. Kifungu sambamba katika Yohana kinatoa maoni ya kuvutia kwamba Yusufu alikuwa mwanafunzi wa "siri" kwa sababu aliogopa viongozi wa Kiyahudi (tazama Yohana 19:38). Hata hivyo, baada ya kifo cha Yesu, alionyesha ushujaa kwa kwenda kwa Pilato ili kuomba ruhusa ya kumzika Yesu.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Yusufu anaelezewa vipi katika habari hii? Unafikiri ni kwa nini hakushirikiana na baraza la Wayahudi kumhukumu Yesu?
3. Je, unafikiri Yusufu anaweza kuwa alijisikiaje alipomwona Yesu akisulubiwa?
4. Yusufu aliupeleka wapi mwili wa Yesu? Alifanya nini ili kuutayarisha mwili wa Yesu kwa ajili ya mazishi?
5. Ni nani waliokuwepo wakati wa kuzikwa kwake Yesu? Kwa nini unafikiri hili linaweza kuwa jambo muhimu?
6. Ungejisikiaje kama ungekuwa pamoja na wanawake hawa waliokuwa wakimfuata Yesu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

## Swali la Matumizi

Mtu ambaye ni "mwanafunzi wa siri" wa Yesu anaweza kutenda jinsi gani?
Je, umewahi kujaribiwa kutenda kama "mwanafunzi wa siri" wa Yesu?
Unaweza kushiriki mfano?

---

Kutazama Mbele

## Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 57: Malaika Kaburini (Luka 23:56-24:7)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Wanawake ambao waliokuja kaburini mapema Jumapili asubuhi walilazimika kungoja siku yote ya Jumamosi nzima kabla ya kuleta manukato ili kuupaka mwili wa Yesu. Hii ilikuwa ni kwa sababu walikatazwa kufanya kazi yoyote katika siku ya "Sabato" (Jumamosi—siku ambayo Wayahudi waliabudu). Je wanaweza kuwa walikuwa wakifikiria nini siku hiyo nzima walipolazimika kungoja? Je, matumaini yao yalikuwa yamefika mwisho? Je, walijaribu kutiana moyo? Je, walijaribu kujua ni nini kilikuwa kimempata Yesu, ambaye walifikiri kuwa ndiye Masihi? Ni mawazo gani wangeweza kuwa kwamba walikuwa nayo walipokuwa wakitembea kuelekea kaburini mapema Jumapili asubuhi?

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Unafikiri wanawake walikuwa wanatarajia kufanya nini Jumapili hiyo asubuhi?
3. Je waligundua nini walipofika kaburini? Je, walikuta nini ndani humo? Je, kama ni wewe ungefanya nini?
4. Wakati wanawake hao wanashangaa, malaika wawili wakatokea. Wanawake wanafanya nini wanapowaona malaika hao?
5. 5. Malaika wanawaambia nini wanawake hao kuhusu Yesu? Je, wanawake waliitikiaje maneno hayo ya malaika?
6. Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wake tena na tena kwamba angekufa na kisha kufufuka. Lakini wanawake hawa inaonekana hawakuelewa tangu mwanzo. Ni mabadiliko gani yalitokea baada ya kukutana na malaika?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, unakumbuka ulifikiri nini mara ya kwanza uliposikia kuhusu ufufuo wa Yesu? Je, kulikuwa na sehemu yoyote ya habari hiyo ambayo ulikuwa na wakati mgumu kuamini?
Je, kuna sehemu yoyote unayopata ugumu kuamini sasa?

---

**Kutazama Mbele**

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 58: Kaburi ni Tupu (Luka 24:9-12)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Ufufuo wa Yesu bila shaka ni tukio muhimu zaidi katika historia ya ulimwengu. Bila ufufuo, Yesu ni mtu mwingine yeyote yule. Kwa kweli, bila ufufuo, Yesu anapaswa kuchukuliwa kuwa mwendawazimu. Hii ni kwa sababu wakati wa maisha yake aliwaambia wanafunzi wake mara kwa mara kwamba angefufuka kutoka kwa wafu, na alijitangaza kuwa Mwana wa Mungu na Mwokozi wa wanadamu. Bila ufufuo, madai ya Yesu ni kama maneno tu ya mtu mwendawazimu. Lakini kwa kufufuka kutoka kwa wafu, Yesu kwa hakika alithibitisha bila shaka yoyote kwamba Yeye alikuwa Mungu kamili na mwanadamu kamili, kama alivyodai kuwa.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.

Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.

Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.

Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Ni jambo gani la kwanza ambalo wanawake hao walifanya baada ya kuona kwamba kaburi la Yesu lilikuwa tupu? Je, jambo hili linatuonyesha walikuwa na hisia za aina gani?
3. Wanafunzi walifanya nini walipopata ripoti ya wanawake hao? Kwa nini walifanya hivyo? Je, wadhani wanawake hao walihisi vipi walipoona jinsi wanafunzi walivyopokea ripoti yao?
4. Kwa kweli Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wake mara nyingi mambo ambayo yangemtokea. Waonelea ni kwa nini hawakumwamini?
5. Ni jambo la kushangaza kwamba Yesu aliruhusu ufufuo wake ujulikane kwanza na wanawake. Je, jambo hili linaashiria nini?
6. Waonelea ni kwa nini Petro alikimbia kufika huko kaburini na kuingia ndani? Je, waona Petro alikuwa na mawazo ya aina gani alipoona kaburi liko utupu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, ukweli wa ufufuo wa Yesu unamaanisha nini kwako binafsi?

Je, jambo hilo limebadilishaje maisha yako?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 59: Yesu Aliyefufuka Awatokea (Luka 24:33-49)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi

Tumezungumza hapo awali juu ya shaka. Katika kifungu hiki Yesu anaonekana kwa wanafunzi wote chumbani, akiwashtua na kuwatia hofu. Mtu angefikiri kwamba wangefurahi kumwona Yesu tena. Badala yake wanakuwa na shaka kwamba ni Yeye kweli. Hakika kuna sababu za mashaka yao. Fikiria mambo ambayo walikuwa wamepitia katika siku tatu zilizopita. Luka anatuambia Yesu, “alifungua akili zao ili wapate kuelewa Maandiko” (mstari 45). Yesu anawahakikishia, na hatimaye wanaamini kwamba yuko hai kweli.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu habari hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Yesu anapowatokea, ni jambo gani la kwanza analolisema? Unafikiri kwa nini anasema hivi?
3. Luka anaandika kwamba mwanzoni wanafunzi walifikiri Yesu ni roho (mzimu). Kwa nini unadhani wanafikiri hivyo?
4. Hakuna anayesema chochote kwa sauti, lakini Yesu anajua wanafikiri Yeye ni mzimu. Je, hiyo inasema nini kuhusu Yesu kwamba alijua walichokuwa wakifikiria na kuhisi?
5. Yesu anashughulikiaje woga na mashaka yao? Je, anawatia moyo wanafunzi wafanye nini ili kuthibitisha kwamba yu hai kweli?
6. Kwa nini unafikiri Yesu anawarudisha kwenye Maandiko ya Agano la Kale ili kueleza jinsi unabii wote kuhusu Masihi ulivyotimizwa ndani yake? Je, hilo linatufundisha nini kuhusu umuhimu pamoja na mamlaka ya Biblia?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Je, tunaweza kujifunza nini kutokana na hadithi hii ili kukabiliana na mashaka yanapokuja katika maisha yetu?

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shirikini pamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.

Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.

Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeaneni katika kikundi chenu.

# Sehemu ya 60: Utume Mkuu na Kupaa Mbinguni (Luka 24:50-53)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi – Jinsi Unavyoweza Kusaidia Kutimiza Agizo Kuu

(Mwombe mtu katika kikundi chako asome Mathayo 28:16-20 katika lugha yake ya mama ikiwezekana.)

Amri ya Yesu kwa wafuasi wake ya kuwaambia wengine ujumbe wa wokovu imekuja kujulikana kama Agizo Kuu. Kila Mkristo ameagizwa kuhusika katika kusaidia kuufikia ulimwengu kwa ajili ya Kristo. Kila mmoja wetu ana jukumu muhimu, alilopewa na Mungu kutekeleza katika kusaidia kutimiza Agizo lake Kuu.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.
Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.
Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.
Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Je, ni amri gani mahususi ambazo Yesu anawapa wanafunzi wake katika Agizo Kuu?
3. Je, agizo hili limekusudiwa kwa wanafunzi pekee, au ni wito kwa waumini wote? Kwa nini ndiyo au kwa nini hapana?
4. Unafikiri ni kwa nini Yesu anatuambia sisi kama wafuasi wake kwamba ana "mamlaka yote mbinguni na Duniani?" Je, hilo linaweza kuwa la maana gani kwetu tunapofanya bidii kumtangazai Kristo kwa wengine na kufanya juhuzi za kuanzisha jumuiya mpya ya kimisheni?
5. Soma Matendo 1:8-9. (Hii ni simulizi nyingine ya Agizo Kuu la Yesu na kupaa kwake mbinguni.) Unafikiri ni kwa nini Yesu aliwaambia wanafunzi wake waanzie kwanza Yerusalemu? Kwa nini hilo lilikuwa jambo muhimu? Kisha Yesu anasema wafanye nini baadaye?
6. Kulingana na kifungu tulichosoma hivi punde kutoka Matendo 1, wanafunzi waliamriwa kupeleka injili kwa nani? Je, hii inaweza kutuambia nini kuhusu jinsi Yesu anavyowaona watu wote?
7. Je, unaweza kufikiria kundi la watu katika nchi yako ambalo linahitaji kusikia injili? Je, unawezaje kuwa wewe ndiwe wa KWENDA kuwaambia kuhusu Yesu?

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Swali la Matumizi

Unawezaje kusaidia kutimiza Agizo Kuu? Kwanza, hakikisha umejitoa (kibinafsi) kwa Kristo na kujazwa na Roho Mtakatifu. Pili, omba Mungu akuongoze. Tatu, Mungu anapojibu maombi yako, panga ni wapi UTAKWENDA. Nne, tafuta mafunzo kutoka kwa Wakristo wengine wakomavu. Tano, chukua hatua na UENDE. Tafuta rafiki Mkristo wa kwenda nawe kushiriki injili na wengine—wao wanamhitaji sana.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shiriki nipamoja katika kikundi chenu jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.

Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.

# Sehemu ya 61: Mwaliko wa Kumjua Yesu Kibinafsi (1 Wakorintho 15:1-4)

Kutazama Nyuma

### Kujaliana sisi kwa sisi

- Kuombeana
- Zungumzeni kutoka kwa ujuzi wa maisha yenu (maswala ya afya, familia, fedha, mahitaji ya kiroho, michezo, nk.)

### Furahini kwa pamoja

- Kwa wimbo, muziki, pambio au shuhuda
- Ibada

### Panga maono kwa ajili ya kikundi chako na kwa kila mmoja

- Ili tuwe wafuasi bora zaidi wa Yesu
- Ili jamii yetu imkaribie Mungu zaidi

### Utoaji na Kushirikiana

- Toa kitu kinachoonekana kutoka kwa yale Mungu amekupa ili kuwasaidia wengine

---

Kutazama Juu

### Utangulizi – Jinsi Unavyoweza Kuhakikisha Kwamba Wewe Ni Mkristo

“Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko;” (1 Wakorintho 15:3-4).

Kwa karne nyingi tangu Yesu aishi Duniani, mamilioni ya watu wamemwalika Kristo maishani mwao. Hata hivyo, wengi wao wamefanya hivyo tena na tena kwa sababu hawajawa na uhakika wa wokovu wao. Hawajakuwa na uhakika wa uwepo wa kudumu wa Kristo, hawana uthibitisho kwamba, kama wangekufa leo, wangeenda kuwa pamoja na Bwana mbinguni. Je, una uhakika na wokovu wako? Jua kwamba kujikabidhi kwako kwa Kristo kunahusisha mambo yote matatu: akili, hisia na nia.

Hatua ya 1: Tazama sehemu hii mara mbili.

Hatua ya 2: Mwambie mshiriki wa kikundi kusimulia hadithi ya sehemu hii kwa maneno yake wenyewe.

Hatua ya 3: Ruhusu kikundi kujaza nafasi yeyote katika hadithi iliyosimuliwa au kufanya masahihisho yeyote.

Hatua ya 4: Maswali ya majadiliano:

1. Ni nini ulichopenda zaidi kuhusu hadithi hiyo? Na ni nini kilichokuvutia zaidi?
2. Neno “dhambi” lina maana gani kwako? Yesu alilipaje gharama ya dhambi yako?
3. Mtu anahitaji kuishi maisha ya Kikristo kwa imani, sio kwa hisia. Je, hisia ina nafasi gani katika maisha yako ya Kikristo? Je, ni kwa jinsi gani na lini hisia zaweza kupotosha?
4. Kwa nini unafikiri ni muhimu kuwa na uhakika wa wokovu wako?
5. Shiriki na kikundi hadithi yako mwenyewe ya jinsi ulivyomjua Yesu.

Tuma kodi hii kutazama sehemu hii kwenye simu yako ya kidijitali. Lugha zingine zinapatikana katika tovuti ya Sinema ya YESU (*JESUS* Film).

### Tamati

Kuna kweli nne muhimu unazohitaji kuzielewa ili kuhakikisha kuwa wewe ni Mkristo:

1. Mwenyezi Mungu anakupenda naye anataka kukupanga mpango wa ajabu kwa maisha yako.
2. Mwanadamu ni mwenye dhambi. Dhambi zake zimemtenga na Mungu. Kwa hiyo hajui upendo na mpango wa Mungu kwa maisha yake.
3. Yesu Kristo ndiye ndiye suluhisho la Mungu kwa dhambi zetu. Kupitia kwake pekee tunaweza kumjua kibinafsi na mpango wa Mungu kwa maisha yetu.
4. Inakupasa kumpokea Yesu awe mwokozi na mtawala wako. Ndipo utajua upendo na mpango wa Mungu kwa maisha yako.

Tazama sehemu hii kwa mara nyingine. Ikiwa hujawahi kuwa na uhakika wa wokovu wako, basi wakati huu unapotazama sehemu hii, omba ukiwa na uhakika ili umpokee Yesu. Ikiwa umempokea Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana, unaweza kuwa na uhakika kuwa wewe ni Mkristo kulingana na ahadi za Neno Lake.

---

Kutazama Mbele

### Matumizi

Shiriki pamoja katika kikundi chako jinsi mnavyoamini Mungu angetaka mfanye.
Fanyeni mazoezi ya kusimulia hadithi (kutoka hatua ya 2) mmoja kwa mwingine.
Shirikisha habari ya leo kwa wengine na waalike waje kwenye kikundi chenu wakati ujao.
Maombi
- Tumshukuru Mungu kwa yale tumejifunza leo.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.
- Ombeeni wengine katika jamii yenu.

# Kumjua Yesu

Kuanzisha Jumuiya yako mpya ya Umisheni
v6.5